**MAHAKAMA** yaamuru mali mchungaji wa kanisa zikamatwe

UKURASA 3



**WIZARA** tatu zajitosa sakata Kenya kuzuia mahindi ya Tanzania

UKURASA 2


JUKWAA LA UONGOZI
Suu Kyi: Mwanamama mshindi wa tuzo Nobel na mzoefu wa kizuizini
Ukurasa 14

siasa
JUMATANO MACHI 10, 2021
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukurasa 13
SIKU YA WANAWAKE DUNIANI
Wakumbushana harakati zianzie familia, kisha kupanda ngazi siasa

Mgongano kifamilia, mtoto na wajukuu wa Mfalme Uingereza

• Bibi Eliza hana tabu, shida kuu...; 'Watoswa', wafadhiliwa Marekani

MEGHAN Markle, mke wa mwanamfalme Harry na mkwe wa Malkia, amesema kuna wakati maisha yalimbana na kuwa magumu sana katika familia ya kifalme na 'hakutaka tena kuwa hai' akisema kwamba hakupata msaada hata alipouomba.

Anasema kibaya zaidi ilikuwa wakati mtu mmoja wa familia hiyo alipomuuliza Harry jinsi mtoto watakayemzaa atakuwa na 'ngozi nyeusi.'

Prince Harry, pia alifichua kwamba baba yake Prince Charles, aliacha kuzipokea simu zake, alipogundua kwamba alikuwa na mpango wa kujiondoa kutoka familia ya kifalme.

Wawili hao wamezungumzia masuala mbalimbali ikiwamo ubaguzi wa rangi, uhusiano wao na vyombo vya habari, afya ya akili na mambo katika familia ya kifalme.

Pia walitangaza kwamba mtoto wanayemtarajia hivi karibuni ...

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Machi 10, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580515

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710


# Nyumba 100 kubomolewa

**MAMIA** Dar waingiwa hofu kukosa makazi...*Endelea Uk. 2*



Sehemu ya nyumba 120 zilizo hatarini kubomolewa kwa amri ya mahakama ifikapo Jumanne ya wiki ijayo, katika eneo la Mabibo Kisimani, mkoani Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CCM: Kama si jitihada hizi, tungepoteza majimbo haya

UKURASA 16

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

### MAOFISA WA RUWASA WANUSURIKA KUFA MAJI

MAOFISA watatu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Iringa, akiwamo Mhandisi wa Mkoa wa Iringa, Joyce Bahati, wamenusurika kusombwa na maji baada ya gari...

**UKURASA WA 4**

### NEMC YATANGAZIA KIAMA WAFANYAKAZI

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewataka wafanyakazi wa baraza hilo waliopewa vibali vya kukagua na kusimamia matumizi ya mifuko ya plastiki...

**UKURASA WA 9**

### LATRA CCC YAHIMIZA MATUMIZI TIKETI MTANDAO

BARAZA la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC), limewataka wananchi kuanza kutumia huduma ya tiketi mtandao, kwamba una faida lukuki ikiwamo kuokoa muda na gharama...

## MWALIMU MKUU ANUSURIKA KIFO TUHUMA ZA WIZI VIFAA VYA UJENZI

UKURASA 2

**MICHEZO** MOROCCO NA MBINU MPYA KWA WAMOROCCO CAF LEO UK. 23

**MAONI, KATUNI** UK. 6

# Nyumba 100 kubomolewa Dar

**Na Christina Mwakangale**

TAKRIBANI nyumba 120 za wakazi wa Mabibo Kisimani, Kitalu namba 55 mkoani Dar es Salaam, ziko hatarini kubomolewa kwa amri ya mahakama ifikapo Jumanne ya wiki ijayo.

Nyumba hizo zinazokadiriwa kuwa na wakazi zaidi ya 500, ziko hatarini kubolewa kutokana na kujengwa kwenye eneo ambalo ni mahususi kwa viwanda.

Mwenyekiti wa wakazi hao, Herman Chilipweli, aliliambia Nipashe jana kwamba, wakazi wa eneo hilo wana taharuki kubwa kuhusiana na hukumu hiyo.

Chilipweli alisema wanafanya jitihada za kutafuta mwanasheria ili awasaidie kukata rufani na kuweka zuio la kutekelezwa kwa amri ya mahakama ya ubomoaji wa nyumba zao.

Nipashe pia ilimtafuta Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kisare Makori, ambaye alikiri kuwapo kwa mgogoro huo na kwamba kwa wakati tofauti, alikutana na wakazi hao kuuzungumzia.

Akifafanua zaidi kuhusu mgogoro huo, Chilipweli alisema inadaiwa eneo lilipimwa na serikali mwanzoni mwa miaka ya 1980 na kutengwa kwa ajili ya viwanda.

Hata hivyo, Chilipweli alisema hakuna mtu au taasisi yoyote iliyowahi kuwafidia wenyeji kama sheria ilivyotaka kwa wakazi waliokuwa wakiishi miaka hiyo.

Alisema ni kutokana na hali hiyo, wenyeji waliokuwa wanamiliki maeneo hayo, waliuza viwanja kwa wakazi ambao hivi wanatakiwa kuondoka.

Chilipweli alidai kuwa Kampuni ya Hai Traders iliwahi kudai kumiliki kitalu hicho ingawa haikutenga fedha kwa ajili ya fidia na baadaye wenyeji waliuza eneo hilo kwa Jehangiry Azizi, mwaka 2005.

Alidai kuwa baada ya kuuziwa, Azizi alifanya uthaminishaji alioutia hewa na haukuwekwa wazi, ukionyesha kuwa mwaka huo eneo lilikuwa wazi, likiwa na banda la mlinzi tu.

Chilipweli alidai kuwa Novemba 2019, wakazi ambao ni walalamikiwa walipelekewa wito na Baraza la Ardhi la Wilaya kujibu shauri 728/2019, kwamba walishindwa kutekeleza agizo lililotolewa na Azizi kuwa waondoke kwenye eneo hilo.

"Kufuatana na ukweli kuwa shauri hilo na hukumu vilikuwa na ukakasi, Baraza la Ardhi la Wilaya, iliagiza shauri likasikilizwe upya Baraza la Ardhi la Kata.

"Mwaka jana, Baraza la Ardhi la Kata ya Mabibo lilimwita Azizi shaurini mara tatu kupitia Ofisi ya Mtendaji na kupitia matangazo kwenye magazeti, lakini hakufika na hata kupekeleka mwakilishi wake.

"Shauri hilo lilisikilizwa na kuamuliwa upande mmoja na liliwapa ushindi walalamikiwa ambao ni wakazi," alidai.

Alibainisha kuwa Machi 3, mwaka huu, hukumu ya shauri la msingi ilitolewa na ushindi kupewa Azizi, ikikazia hukumu ya shauri 91/2015 ya Baraza la Ardhi na Makazi la Kata kwa msingi wa maelezo kuwa kwenye hukumu ya Baraza la Ardhi la Kata ya Agosti Mosi mwaka jana.

"Hukumu haikutamka bayana kutenguliwa kwa hukumu ya shauri 91/2015. Hukumu hiyo iliamuru wakazi wabomoe nyumba zao na kukabidhi Plot 55 kwa mlalamikaji ndani ya siku 14.

"Kinyume cha hapo, mlalamikaji atawabomolea wakazi kupitia Kampuni ya Udalali ya Msolopa Auction bila taarifa," Chilipweli alidai. Alidai shauri hilo linafahamika kwa Waziri wa Ardhi, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Kamishna wa Ardhi Kanda, Diwani wa Mabibo, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Ofisa Mipango Miji Ubungo.

**KAULI YA DC**

Mkuu wa Wilaya Ubungo, Makori, alisema anawashauri wakazi hao kuwahi mahakamani iwapo wanadhani haki haikutendeka, ili waweke zuio la ubomoaji kwa utaratibu wa kisheria.

"Mgogoro huu ninaufahamu una sura tatu. Mimi siwezi kuingilia uamuzi wa mhimili mwingine, mahakama ilikwishaamua.

"Ninachoweza kuwashauri wakazi wa eneo hilo, wakiona hawajatendewa haki, kisheria hapo ni kukata rufani na kuweka zuio la utekelezaji," alisema



Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson (wa pili kushoto), akiwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Paul Ntinika (kulia), Mstahiki Meya wa Jiji la Mbeya, Dourmohamed Issa (kushoto) na Mkurugenzi wa Mipango, Mikakati na Uhusiano wa Kitaasisi wa Benki ya Maendeleo TIB, Patrick Mongella, wakinyanyua moja ya mabati 324 yaliyotolewa msaada na benki hiyo, jijini jana, kwa ajili ya kusaidia kuezekea vyumba vya madarasa ya Shule ya Sekondari Itende. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwalimu mkuu anusurika kuuawa

**Na Jumbe Ismailly, IGUNGA**

WATU watatu akiwamo Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Itumba, wilayani hapa, Juvenary Mgabuzi, wamenusurika kuuawa na kundi la zaidi ya wananchi 400 kwa tuhuma za kuiba 'gypsum board' sita za shule hiyo zilizonunuliwa kwa ajili ya kujengea vyumba vya madarasa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule hiyo, Festo Stewart, aliwataja waliokamatwa na jeshi la jadi, maarufu kwa jina la Sungusungu, mbali na Mgabuzi kuwa ni fundi kinyozi Emmanuel Charles, na fundi ujenzi, Hamza Juma, wote wakazi wa kijiji cha Lugubu.

Stewart alisema tukio hilo lilitokea Machi 5, mwaka huu, kati ya saa 8:00 na 9:00 usiku na kwamba alipata taarifa za siri kutoka kwa raia wema kuwa walimwona kijana mmoja aliyemtaja kwa jina la Hamza Juma akitokea maeneo ya shuleni muda wa usiku akiwa amebeba vifaa hivyo kwenye toroli dogo.

Baada ya taarifa hizo, alisema aliwaarifu viongozi wawili, akiwamo Katibu wa Sungusungu, Shabani Mgabe, na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Lugubu Magharibi, Kulwa Mashamba, ambao walikwenda hadi kwa Juma na walipomkuta walimhoji alikozipatia 'gypsum board' hizo.

Hata hivyo, alisema Juma aligoma kutoa ushirikiano kwa viongozi hao ndipo walipompeleka chini ya ulinzi hali iliyomlazimu kuwaambia ukweli kwamba amezipata kwa kushirikiana na mwalimu mkuu na walizitoa shuleni Itumba.

Mwenyekiti huyo alibainisha kuwa baada ya mtuhumiwa kukiri, walimtaka azitoe nje na kudai kwamba alishaziuza kwa fundi kinyozi Emmanuel Charles kwa thamani ya Sh. 100,000 na ndipo usiku huo waliondoka naye mpaka kwa Charles.

Baada ya kufika kwa Charles, alisema walipomhoji alikana kutonunua na ndipo walipopuliza kipenga cha sungusungu na kufika hapo. Alisema baada ya kuona hali hiyo mtuhumiwa alizitoa 'gypsum' hizo zote ndani na kuondoka nazo hadi ofisi ya serikali ya kijiji na sungusungu walimfuata mwalimu mkuu nyumbani kwake na kumchukua hadi ofisi ya kijiji na kumfungia ofisini.

Asubuhi ya siku iliyofuata, alisema huku sungusungu wakiwa na fimbo, mapanga, mikuki na pinde waliwatoa watuhumiwa wote watatu na kuwapeleka uwanja wa mnada ambako waliendelea kuwahoji huku wananchi wakiwaomba viongozi wao wawakabidhi ili wawaue.

Mashamba alisema baada ya kufanikiwa kutuliza yowe, waliwapigia simu viongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Igunga na ndipo walifika eneo hilo na kuwachukua hadi kituo kikuu cha polisi Igunga.

Katibu wa Sungusungu, Shabani Mgabe, aliwasihi wananchi hao kutojichukulia sheria mkononi na baada ya wananchi kukubali, waliazimia kumkataa mwalimu mkuu kuishi kijijini wala kufundisha watoto wao kwa kile walichodai kwamba amekuwa akiihujumu shule yao na pia hana uhusiano mzuri na walimu wenzake.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Lugubu, Daniel Jinge, alipoulizwa juu ya tukio hilo, alikiri kuwapo na kusema watuhumiwa wote wako mahabusu polisi.

Naye Ofisa Tarafa wa Igunga, Shadrack Kalekayo, alithibitisha kukamatwa kwa mwalimu na wenzake wawili huku akisema amemwagiza Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo kupeleka vielelezo hivyo kituo cha polisi na maelezo.

## Wizara tatu zajitosa sakata la mahindi

**Na Romana Mallya**

WIZARA tatu zimejitosa kushughulikia sakata la kuzuiwa kwa mahindi ya Tanzania kuuzwa Kenya.

Kwa mujibu wa Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, wizara hizo ni pamoja na hiyo anayoiongoza, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Siku nne zilizopita, ilizagaa barua kwenye mitandao ya kijamii iliyodai Kenya imezuia mahindi ya Tanzania na Uganda kuingia nchini mwake.

Akizungumza na Nipashe kuhusu sakata hilo, Prof. Mkenda alisema zipo juhudi kubwa zinafanyika na kubainisha kuwa kwa sasa ni mapema kuziweka wazi.

"Kuna Wizara ya Mambo ya Nje ambayo inahusiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ina kanuni zake za namna ya kufanya biashara, huwezi kutoa tamko tu na kusema sitaki kitu fulani, zipo taratibu.

"Hakuna mtu anayeweza kupeleka mmea wala bidhaa za mimea mfano mazao kama mahindi kwenye nchi yoyote bila nchi husika kutoa vibali vya kuingia ndani ya nchi," alisema.

Waziri huyo alisema anaamini malori yaliyozuiliwa, yana vibali vya kufanya kazi na kwamba nchi ina haki ya kuweka utaratibu huo wa vibali kwa ajili ya usalama wa chakula.

"Lakini, usalama wa chakula umewekwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tulitarajia wenzetu wangeweka hivyo kwa sababu uwezekano wa kupima shehena kabla ya kwenda upo, lakini hawajawahi kuweka hivyo, ndiyo maana inashangaza kidogo.

"Wito wetu kwa wafanyabiashara waliokwama, watambue zipo juhudi zinazoendelea na zinaendelea kwa juhudi kubwa kuhakikisha kwamba suala hili linatatulika," alisisitiza.

Prof. Mkenda alisema Jumuiya ya Afrika Mashariki haiwezi kuendeleza biashara endapo nchi moja itatamka bidhaa za nchi nyingine haziwezi kuingia kwake.

"Kwa sababu kuna kanuni, tunajua mahindi yetu ni salama. Hata kama siyo salama, kuna kitu kinaitwa alama ya utambulisho wa bidhaa, wangeweza kuhitaji wakasema kila shehena ikitoka nchi fulani ije na cheti kinachotuhakikisha katika masuala ya usalama, siamini kama tunaweza kufanikisha biashara kwa kwenda rejareja kwa kupiga marufuku biashara za nchi nyingine.

"Wasidhani tunapuuza suala la afya ya chakula, tunalidhamini kuna kanuni tumekubaliana kwa nchi zote za Afrika Mashariki.

"Nchi moja ikiamua haiheshimu kanuni ina maana haitasaidia sana kwa sababu tunafungua uwanja wa kila nchi kusema bidhaa hii siitaki," alisema.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilaya ya Kipolisi ya Ukonga, jijini Dar es Salaam, Mkaguzi wa Polisi Julius Mangure, akimvalisha kofia dereva wa bodaboda alipokuwa akitoa elimu ya utii wa sheria za usalama barabarani bila shuruti kwa madereva wa bodaboda wa Kinyerezi Sokoni, iliyoandaliwa na Chama cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA) Kanda ya Mashariki, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mahakama yaamuru mali za mchungaji kukamatwa

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Ardhi, imemwelekeza mdai Prosper Rweyendera abadilishe maombi yake ya kutaka kumpeleka jela Mchungaji Godfrey Mallasy kwa kushindwa kulipa Sh. milioni 139.

Badala yake, mahakama hiyo imemshauri awasilishe maombi ya kukamata mali.

Amri hiyo imetolewa na Naibu Msajili Safina Semfumko wa mahakama hiyo baada ya mdaiwa Mallasy kushindwa kulipa fedha hizo na kwamba ameomba alipe Sh. milioni 12 wakati mdai akitaka kiasi hicho kilipwe kama ilivyoamriwa na mahakama.

Mchungaji Mallasy alidai kwamba alikutana na wakili wa mdai, Evodius Rutabingwa, kueleza mpango wake wa kulipa deni hilo.

Alidai kwamba kesi ilikuwa ya Kanisa la City Christian Fellowship lililokuwa Sinza Palestina, Ubungo mkoani Dar es Salaam na yeye alikuwa kiongozi lakini baada ya mgogoro huo kumalizika, kanisa lilisambaratika na kubaki yeye peke yake.

Malassy aliomba mdai amsamehe na alipokataa aliomba amlipe Sh. milioni 12 ambapo kwa kila mwezi alitaka kulipa Sh. 200,000 kwa sababu hana kipato kwa kuwa alikuwa anategemea kanisa ambalo kwa sasa halina waumini.

Alidai hivi sasa anapata fedha pindi anapoitwa kwenda kutoa mada.

Wakili wa Mdai, Rutabingwa, alidai ni kweli mdaiwa aliomba kupunguziwa fedha hizo kutoka Sh. milioni 139 hadi Sh. milioni 12.

Alidai kwa mazingira ya kesi mteja wake alikataa na kuomba alipwe kiasi hicho kama ilivyoamriwa na mahakama na akishindwa wanaomba amri ya kumpeleka gerezani.

"Mahakama hii inawashauri mfanye marekebisho ya maombi yenu ya kumpeleka gerezani kwani magereza yetu kwa wahalifu wetu hayatoshi hata kama mteja ana uwezo wa kulipa gharama za kuishi huko au kama kuna mali mfanye marekebisho na ombi la kwanza liwe kukamata mali," alisema Semfuko.

Alisema suala la kwenda gerezani hufanyika endapo mdaiwa hana mali ambapo mdaiwa alidai ana nyumba lakini ni ya familia.

Baada ya kueleza hayo, Naibu Msajili alimtaka mdaiwa kuangalia anafanyaje ili kulipa hilo deni kwa kuwa kesi ipo kwa jina lake.

Aliagiza wafanye marekebisho ili waambatanishe nyumba ya mchungaji huyo ikamatwe kwa ajili ya kulipa deni.

"Wakati hawa wanaendelea kuwasilisha maombi, wewe uangalie namna ya kulipa deni kabla amri ya kukamata nyumba haijatolewa," alisema Naibu Msajili na kuahirisha kesi hadi Aprili 12, mwaka huu.

Aprili, 2016 mahakama iliamuru kanisa hilo liondolewe mara moja na kumwachia mdai eneo lake.

Uamuzi ulitolewa na Jaji John Mgeta na hukumu kusomwa na Msajili Richard Kabate na Malassy aliamuriwa kulipa kodi ya Sh. milioni moja kila mwezi tangu alipoacha kulipa mwaka 2004.

# Kortini kwa madai kumwachisha shule mwanafunzi, kumwozesha

**Na Jumbe Ismailly, IGUNGA**

WATU watatu wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Igunga kwa tuhuma za kumwachisha shule na kumshawishi mwanafunzi wa darasa la sita (jina linahifadhiwa) kufunga ndoa na mwanamume.

Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Alex Kataya, aliwataja waliopandishwa kizimbani katika mahakama hiyo kuwa ni Kwangu Seleli (56), Ndega Salumu (30) na Kwimba Maswala (26) wote wakazi wa Kijiji cha Matundulu, wilayani Igunga.

Kataya alidai mbele ya Hakimu Mkazi Eddah Kahindi kuwa Novemba 04, mwaka jana, majira ya usiku katika Kijiji cha Matundulu, washtakiwa hao kwa pamoja walimwachisha shule mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka 14 anayesoma darasa la sita baada ya kumshawishi kuolewa na mwanamume. Kataya alidai kwamba washtakiwa wote watatu walitenda kosa hilo kinyume cha kifungu 60A (1)(4) cha Sheria ya Elimu Sura ya 353 kama ilivyofanyiwa marekebisho na sheria ndogo No. 4 ya mwaka 2016.

Baada ya kusomewa shtaka, washtakiwa walikana kutenda jambo hilo na wako nje kwa dhamana ya Sh. milioni mbili kila mmoja za maandishi.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Machi 23, mwaka huu, itakapoanza kusikilizwa kwa kuwa upelelezi umekamilika.


## TANGAZO LA MNADA (WAKALI WA MINADA)

**KIBAIGWA AUCTION MART & COMPANY LTD** dalali wa Mahakama, kwa idhini tuliyopewa na **MAHAKAMA YA WILAYA HANANG - MANYARA** katika shauri la Madai Ndoa/Taraka No. 1 ya 2019, tutakuwa na Mnada wa Hadhara wa kuuza Nyumba (4) katika Plot No. 46 Block "L", Plot 147 Block "K" na Kiwanja kimoja kilichopo Plot No. 48, Block "L". Mnada utafanyika tarehe 22/03/2021 siku ya Jumatatu Mtaa wa LAMAY na JORODOM Mjini KATESH, Wilaya ya HANANG.

| Majina ya wenye mali | Mahali ilipo Mali | Aina ya mali husika | Muda wa Mnada | Idadi ya mali |
|---|---|---|---|---|
| NIKODEMUS MUSSA SOKA. | NYUMBA (2) MTAA WA LAMAY NA MBILI MTAA WA JORODOM NA KIWANJA KIMOJA. | NYUMBA 4 ZIPO PLOT No. 46 BLOCK "L" NA PLOT No. 147, BLOCK "K" NA KIWANJA PLOT No. 48 BLOCK "L" | MUDA NI SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | NYUMBA 4 NA KIWANJA KIMOJA. |

**MASHARTI YA MNADA:-**

1. Nyumba zitauzwa kama zilivyo na mnunuzi atawajibika kubadilisha Hati za umiliki wa viwanja kwa gharama zake mwenyewe.
2. Mnunuzi atalipa 25% ya bei ya nyundo ya dalali na 75% iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) tangu tarehe ya mnada, iwapo haitalipwa Mnada unatangazwa upya na fedha ya awali haitarudishwa.
3. Wananchi wote mnakaribishwa kwenye mnada huu wa Hadhara tarehe 22/03/2021 siku ya Jumatatu, Karibuni sana.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na Dalali wa Mahakama kupitia Kampuni ya Kibaigwa Auction Mart & Co. Ltd **0755 706817/0784 718272 za Wadaawa ni 0784 712065 na 0766 987199.**

..............................

**Jeremiah M. Mtagwa**
**DALALI**

# Maofisa RUWASA wanusurika kusombwa na maji Iringa

**Na Francis Godwin, IRINGA**

MAOFISA watatu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Iringa, akiwamo Mhandisi wa Mkoa wa Iringa, Joyce Bahati, wamenusurika kusombwa na maji baada ya gari lenye namba STK STK 6524 aina ya Nissan walilokuwa wakitumia kutumbukia kwenye mtaro wa maji.

Maofisa hao walipatwa na janga hilo walipokuwa katika msafara wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Iringa kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 7:00 mchana katika eneo la Mwandomela, barabara ya Izazi - Pawaga, baada ya dereva wa gari hilo kushindwa kulimudu kutokana na mvua kubwa kunyesha.

Licha ya gari hilo kuzama, hakuna madhara yoyote kwa binadamu zaidi ya gari kuharibika na kukwama eneo hilo kwa zaidi ya saa matatu bila kutoka hadi lilipovutwa na trekta.

Kutokana na ajali hiyo, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Iringa, Dk. Abel Nyamahanga, na wajumbe wake walisitisha kwa muda ziara hiyo kwa ajili ya kusaidia kulitoa gari hilo katika eneo hilo ambalo ni mbali na makazi ya watu.

Akizungumzia miradi hiyo ya maji iliyokaguliwa, Dk. Nyamahanga aliwataka viongozi wa jumuiya za watumia maji kupitia miradi ya RUWASA, kuhakikisha wanasimamia miradi hiyo pamoja na kuhimiza wananchi kulipa bili za maji kwa wakati ili kuwezesha miradi hiyo kufanyiwa matengenezo pindi inapoharibika.

Dk. Nyamahanga alisema kazi inayofanywa na RUWASA katika wilaya ya Iringa na mkoa ni kubwa na kamati yake imeridhishwa na ujenzi wa miradi hiyo ambayo wameitembelea na hata kama kuna kasoro, ni zile za kawaida ambazo zilijitokeza kabla ya serikali kuanzisha RUWASA.

Pia alisema miradi hiyo inapaswa kulindwa ili kuwezesha wananchi zaidi kupata huduma ya majisafi na salama kama ilivyo dhamira ya serikali kuhakikisha inamtua mama ndoo kichwani, hivyo iwapo jumuiya hizo za watumia maji zitashindwa kulinda miradi hiyo, kuna uwezekano wa miradi kufa.

"Serikali imejipanga kupambana na changamoto mbalimbali za wananchi kwa kuzifanyia kazi ikiwamo ya maji vijijini na kazi hiyo inaendelea kutekelezwa kwenye maeneo mbalimbali," alisema.

Mhandisi wa RUWASA Mkoa wa Iringa, Bahati, alisema RUWASA inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji katika wilaya zote za mkoa wa Iringa lengo likiwa ni kupunguza kama si kumaliza kabisa kero za maji kwa wananchi vijijini.



Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Iringa, wakiongozwa na Mwenyekiti wa chama hicho mkoa, Dk. Abel Nyamahanga (kulia), wakisaidiana kulinasua gari lenye namba STK 6524 aina ya Nissan, lililokuwa na maofisa wa RUWASA, baada ya kutumbukia kwenye mfereji wa maji ya mvua, wakiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maji, mkoani humo juzi. P**ICHA: FRANCIS GODWIN**

# NEMC yatangazia kiama wafanyakazi

**Na Richard Makore, MWANZA**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewataka wafanyakazi wa baraza hilo waliopewa vibali vya kukagua na kusimamia matumizi ya mifuko ya plastiki, kuacha kuihujumu serikali kwa kushindwa kudhibiti bidhaa hizo zisiendelee kutumika katika jamii.

Katazo la matumizi ya mifuko hiyo lilitolewa na serikali mwaka 2019 kwa lengo la kulinda mazingira katika mito, maziwa na juu ya ardhi kwa kuwa athari zake ni kubwa.

Baraza hilo limesikitishwa na kuitaka jamii na Watanzania kukataa kutumia mifuko isiyoruhusiwa ambayo inaingizwa kwa njia za panya kutoka nchi jirani na kuuzwa soko la hapa nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Mwanza, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, aliwaonya watumishi wa baraza hilo kuacha tabia ya kushirikiana na wahalifu kuhujumu juhudi za serikali katika kupambana na matumizi ya mifuko hiyo.

"Dhamana mliopewa ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya mifuko isiyoruhusiwa ni kubwa na msishirikiane kwa namna yoyote na wahalifu wanaoingiza mifuko hiyo nchini," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema baraza lake ambalo limepewa dhamana ya kupambana na matumizi ya mifuko hiyo, halitaki kuona vifungashio vyovyote vilivyokatazwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema Tanzania si mali ya mtu mmoja hivyo kila mmoja anayo haki na wajibu wa kulinda ardhi yake kwa kuacha kutumia mifuko ya plastiki isiyoruhusiwa.

Aliomba jamii kukataa kutumia mifuko isiyoruhusiwa na kutoa taarifa kwa mamlaka husika ili wahalifu wakamatwe na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Wiki iliyopita NEMC kwa shirikiana na taasisi zingine za serikali walikamata shehena ya vifungashio visivyoruhusiwa ambavyo viliingizwa nchini kwa njia ya panya katika eneo la Busweru wilayani Ilemela mkoani Mwanza.

# Waliojenga mabondeni waamuriwa kuondoka

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

WAKAZI wa maeneo ya Omukigusha na Buyekera yaliyoko kandokando mwa Mto Kanoni katika Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera wametakiwa kuhama katika maeneo hayo ili kuepuka mafuriko.

Wametakiwa kuondoka katika maeneo hayo hatarishi na kwenda sehemu salama katika msimu huu wa mvua za masika.

Akizungumza na Nipashe Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Deodatus Kinawiro, alisema kila msimu wa mvua nyumba za wananchi wanaoishi katika maeneo hayo hujaa maji na kusababisha wananchi kushindwa kutoka hali inayosababisha serikali kwenda kuwaokoa kwa mitumbwi.

Kinawiro alisema kuwa kwa mara tatu mfululizo serikali imekuwa ikipeleka mitumbwi katika maeneo hayo kuokoa wananchi waliozingirwa na maji na kuwataka kutoa ushirikiano kwa kuhama mapema ili kuokoa mali na maisha yao.

"Mungu alisaidia katika msimu hiyo tuliyopeleka mitumbwi kuokoa watu kwa mara tatu mfululizo hakikutokea kifo, lakini hilo halizuii kujiandaa mapema kukabiliana na athari za mvua kwa wananchi wa Omukigusha na Buyekera, pia maeneo ya Nyamkazi yaliyoko kando kando mwa Ziwa Victoria," alisema.

Alisema kuwa kwa bahati mbaya wananchi katika maeneo hayo walijenga kufuata Mto Kanoni miaka ya nyuma kutokana na baadhi ya wasimamizi wa sheria kushindwa kuisimamia ipasavyo.

"Wito wangu kwa wananchi waache kujenga katika maeneo hatarishi yakiwamo ya mabondeni na kando kando mwa mito, wafuate ushauri wa wataalamu wa mazingira ili kuepuka kukumbwa na madhara," alisema.

Baadhi ya wakazi wa eneo la Omukigusha akiwamo Focus Sylvester waliomba serikali kuwasaidia kutengeneza mitaro imara kwa kutumia mawe ili mkondo wa maji utakapopita usimomonyoe udongo na kusababisha maji kuingia katika nyumba zao.

"Tumejitahidi kuchimba mitalo ambayo tunaisafisha mara kwa mara lakini siyo imara. Tukijengewa mitaro imara tutapunguza tatizo," alisema.

HABARI KITAIFA

# DK. Tulia apigia debe maendeleo elimu

**Na Romana Mallya**

NAIBU Spika wa Bunge, Dk. Tulia Acskon, ametoa wito kwa wadau, zikiwamo benki kuchangia sekta ya elimu ili kuwawezesha watoto wanaofaulu kidato cha kwanza kusoma bila tatizo.

Dk. Tulia alitoa wito huo jana wakati akipokea msaada wa mabati 324 kutoka Benki ya Maendeleo ya TIB ambayo yatatumika kuezeka Shule ya Sekondari Itende jijini Mbeya.

Msaada huo ulikabidhiwa na Mkurugenzi wa Mipango, Mikakati na Uhusiano wa Kitaasisi wa benki hiyo, Patrick Mongella.

Dk. Tulia ambaye ni Mbunge wa Mbeya Mjini, alisema mchango huo unaunga mkono jitihada za Rais, John Magufuli za kuendeleza kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu ili kutoa maarifa na ujuzi wa kutosha kwa wahitimu.

Aliishukuru benki hiyo kwa msaada huo kwa kata ya Itende ambayo haina shule ya sekondari na kusababisha watoto kwenda umbali mrefu kuitafuta.

Dk. Tulia amewaomba wadau na benki nyingine nazo zijitokeze ili kuzisaidia kata nyingine ambazo nazo hazina shule za sekondari kama vile kata ya Izawa na Kata ya Itagano zote za mkoani humo.

Mongella alisema msaada huo utaondoa matatizo ya wanafunzi kutembea umbali mrefu kutafuta elimu ya sekondari.

Alisema wameutoa kwa kutambua ustawi wa sekta ya elimu katika Manispaa ya Jiji la Mbeya na Taifa kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Mongella, elimu ni moja ya maeneo wanayoyaunga mkono ndiyo maana wametoa msaada huo ili kukamilisha miundombinu ya elimu kwa wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza.

"Tunaamini msaada huu utachangia malengo ya serikali ya kuendelea kuboresha elimu inayotolewa ili iweze kutoa maarifa na ujuzi wa kutosha kwa wahitimu katika nyanja zote za elimu," alisema.



# RC ataka thamani ya fedha miradi maji

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, ameutaka Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kuhakikisha miradi inayotekelezwa inakuwa na ubora.

Sambamba na hilo, ametaka miradi hiyo kuendana na thamani halisi ya fedha zinazotumika.

Ndikilo alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akizungumzia masuala ya hali ya maji katika mkoa na RUWASA.

Alisema RUWASA inatakiwa kusimamia kikamilifu miradi ya maji itekelezwe na ikamilike kwa wakati kulingana na mkataba ili iwasaidie wananchi ambao wana kero ya kupata huduma hiyo.

Ndikilo alisema utekelezaji wa miradi hiyo umo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), hivyo ni vyema ikasimamiwa vizuri kuwaondolea usumbufu wananchi ambao bado hawajapata huduma ya majisafi na salama.

Pia aliwataka wananchi kuwa makini na sehemu ya kutupa taka ambazo katika maeneo mengine zimekuwa chanzo cha kuharibu vyanzo vya maji.

"Taka zihifadhiwe vizuri zisiathiri vyanzo vya maji. Kila mmoja awe mlinzi, tusiache jukumu hili kwa serikali kwani waathirika ni sisi ambao tunapata taabu baadaye," alisema.

Ndikilo alisema mkoa huo unalenga kufikisha huduma ya maji kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa kwa asilimia 84 vijijini na 95 kwa mijini.




Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani akiwa amepanda bodaboda huku akiwa hajavaa kofia ngumu 'helmet' katika Barabara ya Morogoro, eno la Ubungo Kibo, jijini Dar es Salaam juzi, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Duka leteketea, mlinzi akutwa amefariki dunia

**Na Joctan Ngelly** GEITA

DUKA la biashara ya nguo, mabegi na viatu limeteketea kwa moto eneo la Nyankumbu mkoani Geita.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Zabrone Muhumha, alisema tukio hilo lilitokea jana majira ya saa 11:14 alfajiri.

Muhumha alisema askari wa Zimamoto na Uokoaji wakiongozwa na Mkaguzi Msaidizi Fidel Wambura, walifika eneo la tukio saa 11:20 alfajiri wakiwa na gari lenye namba za usajili STL 2188 HINO RANGER kwa ajili ya kuzima moto huo.

Alisema askari hao walipofika eneo la tukio, walikuta duka hilo likiungua na walifanikiwa kuuzima huo moto, lakini hakuna kitu chochote kilichotolewa katika duka hilo linalomilikiwa na Juma Edward.

Hata hivyo, alisema moto huo hakusababisha madhara sehemu zingine na hakuna madhara yoyote kwa binadamu kutokana na moto huo.

Aidha, alisema uchunguzi wa awali wa moto huo unaonyesha kuwa huenda chanzo cha moto huo ni hujuma baada ya kukuta mlinzi wa duka hilo, Obadia Masele, amefariki dunia kwa kupigwa na kitu chenye incha kali na watu wasiojulikana.

Mhumha alisema mlinzi huyo alikutwa umbali kama mita 40 kutoka eneo la tukio na mali zilizoteketea kwa moto huo bado thamani yake haijajulikana na uchunguzi unaendelea.

Kamanda huyo aliwataka wananchi hasa wamiliki wa maduka mkoa wa Geita wawe na vifaa vya kuzimia moto na wawe na walinzi wa kutosha wenye mafunzo ya kijeshi ili kuweka usalama katika maduka yao.

Aliwataka baadhi ya wafanyabiashara wa maduka kuacha tabia ya kuweka mlinzi mmoja wa kulinda maduka mengi badala yake kila mwenye duka awe na mlinzi wake ili kuimarisha ulinzi.

Pia Kamanda Muhumha aliwataka wamiliki wa kampuni za ulinzi katika mkoa wa Geita kuwapeleka askari wao kwenye ofisi za jeshi hilo, ili kupewa mafunzo ya kuzima moto pindi unapotokea katika maeneo yao ya kazi.Mhumha alizionya kampuni zitakazokiuka agizo hilo kwamba zitachukuliwa hatua kali za kisheria.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mifumo muhimu kukabili rushwa ya ngono vyuoni

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani juzi, Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU), ilitoa matokeo ya utafiti wa rushwa hiyo kwenye Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam (UDSM), yakionyesha vishawishi na kiwango.

Aidha, alieleza wanafunzi waliohojiwa asilimia 58 na watumishi asilimia 69 kuwapo kwa matukio ya vitendo vya rushwa ya ngono.

Pia,walieleza visababishi ni kutoa alama za chini kwenye mitihani, vitisho vya kutofaulu kwa mwanafunzi, kutoa ahadi kama kumpatia ajira, cheo na chumba cha kuishi chuoni.

Nyingine ni nafasi ya uongozi, kuongezewa alama za ufaulu au kusaidia kupata ufadhili wa masomo, kuchelewesha utoaji wa huduma na wahadhiri kuwaita wanafunzi kwenye mazingira yasiyo rasmi kwa ajili ya kukagua kazi zao.

Haya yameonekana kwenye vyuo viwili, lakini tunaamini ukifanyika utafiti kwenye vyuo vingine yataibuka ambayo kwa namna moja au nyingine ni kikwazo kwa ustawi wa jamii kwa kuwa rushwa hiyo ipo kwa wanaume na wanawake.

TAKUKURU imeeleza kuwapo kwa mifumo dhaifu ya kudhibiti matumizi mabaya ya mamlaka, kusimamia uwajibikaji na ajira hasa za wahadhiri.

Ni muhimu sana mamlaka husika zikajenga mifumo imara ambayo itawezesha kukabiliana na tatizo la rushwa ya ngono, kwa kuwa inawezekana kuwapo utaratibu na uwajibikaji na kuzuia wenye mamlaka kuyatumia vibaya.

Wanafunzi wa kike na kiume wamejikuta katika wakati mgumu, huku baadhi wakiharibiwa maisha yao kwa kunyimwa alama ambazo walizistahili, lakini kutokana na visa vya baadhi ya wahadhiri kutaka uhusiano wa kingono nao, basi wanakuwa kikwazo kwao, kiasi cha wengine kurudia masomo au mwaka.

Wapo ambao wamelazimika kuacha vyuo baada ya kukumbana na usumbufu mkubwa, huku baadhi ya wahadhiri wakishindwa kutimiza wajibu wao kikamilifu kutokana na manyanyaso ya kingono.

Kutokana na uchache wa vyumba vya malazi kwa wanafunzi wamejikuta kwenye mtego wa kutoa rushwa ya fedha na ngono ili kupata huduma hiyo ambayo sasa imegeuka kuwa fimbo katika baadhi ya vyuo.

Mathalani, katika chuo kimoja (jina limehifadhiwa) jijini Dar es Salaam, mwanafunzi alizungushwa wiki mbili kupata namba ya kulipia chumba licha ya kupata chumba hadi mzazi wake alipoingilia kati na kuwekana sawa na wasimamizi wa hosteli hizo na mwanafunzi kupatiwa chumba.

Maana yake yanatengenezwa mazingira magumu kiasi cha mwanafunzi kuamua kutoa fedha au la, na kama anashindwa kupata fedha, basi wanatoa rushwa ya ngono.

Ni muhimu TAKUKURU ikaweka mfumo wa ufuatiliaji kwenye vyuo, ili wanafunzi waripoti vitendo wanavyofanyiwa, na hilo linawezekana kwa kutumia teknolojia ambayo kunaweza kuwa na mfumo ambao mwanafunzi anaripoti jambo bila kujulikana na baada ya hapo hatua zinachukuliwa kwa muhusika.


Lakini ni muhimu sana vyuo vikazungumzia suala hili kwa uwazi kupitia midahalo na mikutano mbalimbali, kwa kuwa kuna mchanganyiko wa wanafunzi kutoka vijijini na mjini, na waathirika wakubwa huwa ni waliotoka vijijini au amelelewa katika mazingira ya kimaadili yasiyowafanya wawe na tabia mbaya.

Kuendelea kwa vitendo vya ngono ni kuua ndoto za wanafunzi wengi, ambao ni taifa la kesho, hivyo ni muhimu sana kuchukua hatua madhubuti kukabili suala hili.

Pia mifumo ya ajira iwe wazi kupitia Tume ya Ajira, kuliko kuwaumiza kisaikolojia wanaotafuta ajira na wanafunzi, kwa kuwa ni heri kujua umekosa au kufeli masomo kutokana na uwezo mdogo, lakini siyo kwa sababu hukutoa rushwa kwa mtu fulani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






Na Christina Mwakangale

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kinamama siku na idadi yetu, chachu kunyanyuka

IPO mikataba mbalimbali ya kimataifa na miongozo ambayo Tanzania iliridhia kuitekeleza kikanda, ikiwamo Tamko la Shirika la Maendeleo la Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) la mwaka 2005.

Pia imeridhiwa na kutafsiriwa kitaifa ndani ya 'sheria mama' ambayo ni Katiba ya Tanzania. Hii ni pamoja na Tamko la Haki za Binadamu la mwaka 1948.

Upo Mkataba wa Kimataifa Kuhusu haki za wanawake za Kisiasa wa mwaka 1952 na Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW 1979).

Mikataba hiyo imeweka kiwango cha uwakilishi wanawake kufikia asilimia 50 kutoka 30.

Ikiwa ni siku moja tangu dunia iadhimishe Siku ya Wanawake Duniani, inayoadhimishwa kila mwaka, Machi 8, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo anaukumbusha umma kutoa fursa kwa wanawake kutoa maamuzi.

Anasema, pengine kungekuwapo mafunzo ya namna ya wanawake kushika nafasi za uongozi basi yangeanza mafunzo kuhusu kuondokana na kasumba kwamba mwanamke hawezi kuongoza.

Samia anasema, pia yatolewe mafunzo kwa wanawake jinsi ya kupata nafasi kushika nafasi ili kuongeza ushiriki wao katika uamuzi na jitihada zinahitajika, anasema Samia na kwamba ili kuhakikisha wanawake wanaongezeka kwenye nafasi za uongozi, kwa kuwa bado kuna tatizo.

Kadhalika, anawataka wanawake kila wanapozungumza mambo yao na kupanga kutatua changamoto na kuondoa vikwazo, waache kulalamika bali wayatatue.

Anatoa wito kuchukuliwa hatua, huku wanaume wakishirikishwa katika kuamua namna ya kuongeza nafasi za uongozi wa wanawake kwa kuwa walioshika nafasi za maamuzi zaidi ni wanaume.

Samia anasema, duniani kote mwanamke kwa kiwango cha juu wamezungukwa na madhila tofauti na kumkwamisha maendeleo yake hasa umaskini.

Anasema, Katiba ya Tanzania inatoa usawa wa mwanamke na mwanaume, hivyo katika kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ni sawa na kuhusu fursa za kiuchumi, kisiasa anataja ulipo usawa na kwamba Tanzania ijikite katika kumwondolea mwanamke vikwazo.

Anasema mwanamke ni nguzo inayopaswa kujengwa kwa madhubuti ili kupata maendeleo, Makamu wa Rais Samia, anasema mazingira wezeshi kwa wanawake ni nguzo pekee,

Katika takwimu anazozitaja ni kwamba wanawake wanaweza kuwa chachachu ya maendeleo ni kutokana na kuwa Tanzania ina wanawake asilimia 51 na wanaume ni 49.

Katika idadi hiyo, Samia anasema wanawake nchini wawe chachu na mwanzo wa mageuzi katika maendeleo kupata uongozi kuifikia dunia yenye usawa.

Anasema Machi 4, mwaka huu, alishiriki kikao kuhusu uongozi nchini na mazungumzo yakawa kwamba mbinu za kumwezesha mwanamke kuingia kwenye uongozi yalisisitizwa.

Samia anasema, kwa kuwa wanaume ndio walioshika nafasi za maamuzi ni wengi, washirikishwe kwenye vikao vya wanawake ili kuleta mabadiliko ya kiuongozi na kuongeza idadi ya wanawake.

Anasema maazimio 12 ya Beijing yamefanikiwa ingawa kuna mkwamo katika baadhi ya meneo ikiwamo umaskini.

Anasema kuhusu elimu kuna mafanikio makubwa nchini, ikiwamo kutolewa elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi sekondari ni ukombozi kwa wanawake, ambao ndio wanotarajiwa kuja kuwa viongozi baadaye.

Samia anasema, pamoja na baadhi ya wasichana kutomaliza elimu na masomo ipo fursa ya kujiunga na vyuo vya ufundi ambavyo vipo kwenye mikoa nchini na kuwapatia ujuzi.

Kuhusu afya anasema kuna ongezeko la zahanati, hospitali na vituo vya afya na kufanya huduma kuwafikia kinamama na watoto, ambao huwa waathiriwa wakubwa huduma hizo zikiwa duni.

Anasema haki kisheria kwa wanawake sasa inapatikana, ingawa udhalilishaji, unyanyasaji kwa wanawake ni tatizo kubwa ambalo bado linahitaj jamii na madawati ya kushughulikia hilo kuongezwa.

Katika uchumi, anasema kuna mazuri mengi ingawa kunahaja ya kuongeza mazingira wezeshi ya shughuli za kibiashara, ili kuntunza kaya kwa kuwa wanawake ni wakuu wa kaya.

Anasema hivi sasa katika uongozi, kuna nafasi nyingi za kisiasa kuna wanawake zikiwamo makamu wa rais, naibu spika na mawaziri na pia kwenye bodi wapo wanawake.

Samia anasema, mchango wa wanawake na utolewaji maamuzi sahihi, unategemeana na usawa wa jinsia ili kuondoa upendeleo wa upande mmoja.

HABARI KITAIFA

# Lukuvi aagiza waliokwamisha urasimishaji wachukuliwe hatua

**Na Munir Shemweta, WANMM**

WAZIRI Lukuvi ameagiza kuchukuliwa hatua na kuchunguzwa watendaji wote wa Chuo cha Ardhi Morogoro waliochelewesha na kusababisha urasimishaji makazi katika Kata ya Kivule, Dar es Salaam.

Pia ameagiza makamishna wote wa ardhi katika ofisi za ardhi za mikoa kumpatia majina na kampuni zilizoshindwa kutekeleza kazi za urasimishaji huku zikiwa zimechukua fedha za wananchi.

Lukuvi alitoa maagizo hayo juzi alipozungumza na wananchi wa Kata ya Kivule, alipokwenda kushughulikia kero ya urasmishaji kwenye eneo hilo.

"Watumishi wote waliosababisha kuchelewesha urasimishaji hapa Kivule wachukuliwe hatua kali na uchunguzi ufanyike dhidi yao kwanini wanatutukanisha katika jambo hili," alisema Lukuvi.

Alisema tatizo hilo halikufanywa na serikali bali ni majambazi wawili watatu na wizara yake haiko tayari kuvumilia uhuni uliofanywa. Alizitaka kamati zote za urasimishaji kusimamia vizuri zaoezi hilo huku akisisitiza kuwa kazi wanayofanya ni ya kujitolea na siyo ya kujilipa fedha.

Kwa mujibu wa Lukuvi, wizara haiwezi kuacha jambo kama hilo lililopata baraka kutoka kwa Rais John Magufuli liachwe bila kuchukua hatua dhidi ya watu wachache wanaohujumu.

Alimwagiza Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mary Makondo, kuchukua hatua dhidi ya watumishi wa Chuo cha Ardhi Morogoro ambacho kiko chini ya wizara na kuanza uchunguzi mara moja kujua fedha zilizotolewa kwa kazi hiyo zimekwenda wapi.

Aidha, Lukuvi alikiagiza Chuo cha Ardhi Morogoro kuanza urasimishaji makazi kwa wakazi wote 20,000 wa Kivule na kazi hiyo ikamilike kufikia Juni 30, mwaka huu, sambamba na kuwataka wananchi waliowekewa alama (vigingi) kukamilisha malipo ili kupatiwa hati.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Urasimishaji katika kata ya Kivule, wananchi 3,446 wamechangia zaidi ya Sh. milioni 534 kwa ajili ya kufanyiwa urasmishaji lakini kazi hiyo imeshindwa kufanyika tangu mwaka 2017 na kati ya hao, waliopatiwa hati ni 22 pekee.

"Zoezi (kazi) limechelewa (imecheleweshwa) na waliopewa kazi hiyo wamefanya vibaya sana na kuhoji chuo kinachofundisha wataalam wa ardhi, inakuwaje kinaonyesha mfano mbaya?" Alihoji Lukuvi.



Wafanyakazi wa kampuni ya CRJE, wakiendelea na ujenzi wa barabara ya Mtaa wa Pile kwa kiwango cha zege katika Manispaa ya Temeke, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TBS yaongeza kasi ukaguzi wa majengo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAGUZI wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) wameongeza kasi ya kufanya ukaguzi wa majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi yaliyopo Kawe Ukwamani na Mzimuni, Kinondoni jijini Dar es Salaam ili kuwakumbusha wajibu ili kulinda afya za walaji.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkaguzi wa TBS, Venance Colman, alisema kwa mujibu wa sheria, majengo yanayouza bidhaa za chakula na vipodozi, yanatakiwa yasajiliwe kwa sababu yanahifadhi bidhaa ambazo zina athari ya moja kwa moja kwa mtumiaji, hivyo inabidi yafuatiliwe ili kuangalia namna bidhaa zinavyohifadhiwa.

Colman alisema bidhaa hizo zikihifadhiwa vibaya, zinaweza kuharibika haraka na uhifadhi wake unaweza kusababisha bidhaa kuchafuliwa na wadudu au vimelea ambavyo vinaweza kusababisha mtumiaji akapata madhara ya kiafya moja kwa moja.

"Kwa hiyo TBS imepewa jukumu hilo. Jukumu mojawapo ni kufanya ukaguzi na kusajili maduka, stoo, baa na kwa ujumla maeneo yanayohusika na bidhaa za chakula na vipodozi," alisema Colman.

Alisema wanafanya hivyo ili kuwakumbusha wafanyabiashara wajibu wao huo, hasa kwa kuzingatia kuwa kabla ya mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2019, jukumu hilo lilikuwa chini ya iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA).

Alisema kufuatia mabadiliko hayo wametoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari, lakini kutokana na wafanyabiashara wengi kuwa na majukumu mengi, wapo ambao walikuwa hawajui waende wapi kusajili majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi.

"Kwa hiyo, tunawaelekeza jinsia ya kupitia kufanya usajili, kwa sababu sasa hivi unafanyika kwa njia ya mfumo unaoitwa Online Application System, kwa hiyo tunawaelekeza jinsi ya kuingia kwenye huo mfumo na kufanya huo usajili," alisema Colman.

Alisema mteja akishatuma ombi lake linakwenda TBS na kisha litachakatwa na itafikia sehemu anapewa namba maalum kwa ajili ya kufanya malipo.

"Akishalipia mkaguzi atatumwa kwenda kufanya ukaguzi kuangalia na kumwelekeza namna ya kuzihifadhi bidhaa zake kulingana na matakwa ya uhifadhi chakula na vipodozi," alisema Colman.

Kwa mujibu wa Colman pale mwombaji anapokidhi vigezo anapewa cheti ambacho kinadumu kwa mwaka mmoja na baada ya kipindi hicho, atakuwa akikihuisha.

"Kwa hiyo atakuwa anatembelewa na wakaguzi wa TBS sio chini ya mara mbili kwa mwaka ili kuweza kuangalia jinsi anavyoendesha biashara yake na kama anakidhi matakwa ya kiafya ya hizo bidhaa," alisisitiza Colman.

Alifafanua kwamba ukaguzi huo ulikuwa unafanyika tangu majukumu ya iliyokuwa TFDA yalipohamishiwa TBS, lakini wale wateja waliokuwa na uelewa na mabadiliko ya sheria hiyo walikuwa wanatuma maombi wenyewe kwenye shiria hilo.

"Kwa hiyo katikati ya hao, wengi tunaowakuta wana vyeti vya usajili wa majengo na bidhaa za vyakula na vipodozi, lakini bado wapo ambao hawana uelewa wafanyeje na badala yake walikuwa wakisubiri watu wawafuate dukani kwa ajili ya kuwaelekeza kwa sababu hawana muda wa kutosha kwenda TBS kufuata huduma hiyo," alisema Colman.

# Benki ya UBA yaja kidigitali

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya UBA Tanzania imesema inalenga kuboresha zaidi huduma zake ili kuhakikisha wanawanufaisha zaidi wananchi hususani huduma za kidijitali.

Akizungumza wakati wa kuzindua programu mpya inayojulikana kama UBA Mobile APP, Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kidijitali wa benki hiyo, Asupya Bussi, alisema huduma hiyo inalenga kuboresha zaidi huduma za benki hiyo kwa njia ya mtandao pamoja na kukuza huduma za kifedha kidigitali.

Bussi alisema huduma hiyo inawalenga zaidi wamiliki wa akaunti katika benki hiyo na wanaotarajiwa kufungua.

"Hii 'application' inakuja na maboresho zaidi ambayo yanasaidia maisha kuwa rahisi kwa wateja wetu na hutoa chaguzi nyingi za kudhibiti, kuomba msaada au kwa namna yoyote ambayo mtumiaji anataka," alisema Bussi.

"Ina kielelezo tofauti pamoja na muundo wa kisasa kwa watumiaji tofauti na inawapa vitu muhimu ikiwamo vya kufurahisha."

Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa benki hiyo nchini, Brendansia Kileo, alisema programu hiyo mpya ilitengenezwa ili kuongeza ufanisi, kupunguza gharama kwa wateja pamoja na kukuza uhusiano.

"Pia inaimarisha usalama zaidi katika mfumo wa malipo na wateja wanaweza kufanya shughuli zao malipo popote walipo, inamrahisishia mteja asipoteze muda wake na kufanya shughuli zake nyingine za maendeleo," alisema Kileo.

"Uwekezaji ambao tumefanya kwenye sekta ya teknolojia kwa sasa umeanza kuzaa matunda na malengo ya benki ni kuwa inayoongoza kwa huduma za kidigitali barani Afrika."

**"Hii 'application' inakuja na maboresho zaidi ambayo yanasaidia maisha kuwa rahisi kwa wateja wetu na hutoa chaguzi nyingi za kudhibiti, kuomba msaada au kwa namna yoyote ambayo mtumiaji anataka," alisema Bussi.**

# Mbunge: Vita kupinga ukatili ya kila mtu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood, ameitaka jamii kupiga vita ukatili wa aina zote, ili kufikia malengo ya kuwa na kizazi chenye usawa kati ya wanawake na wanaume.

Abood alitoa wito huo juzi alipokabidhi hundi ya Sh. milioni moja kwa kina mama wa Jukwaa la Wanawake wa Kata ya Mazimbu, Manispaa ya Morogoro wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Mbunge huyo alisema jamii inapasa kutambua usawa kati ya mwanaume na mwanamke katika nafasi mbalimbali za kijamii na uongozi.

Aliwataka wanawake katika kata zote Manispaa ya Morogoro kuchangamkia mikopo inayotolewa na serikali isiyo na riba ili kujikwamua kiuchumi kupitia shughuli za ujasiriamali na kujiletea maendeleo.

Mbunge huyo pia alitoa ahadi ya kuchangia madawati 56 kwa kitengo maalum cha watoto wenye ulemavu katika Shule ya Msingi Mazimbu (A) kufuatia Jukwaa la Wanawake Kata ya Mazimbu kuchangia madawati manne kwa wanafunzi hao.

Aliahidi kutoa msaada wa kiti kimoja cha magurudumu matatu kwa ajili ya mtoto mwenye ulemavu wa viungo ambaye ni mwanafunzi ili usafiri huo umrahisishie kufika kwa wakati shuleni na kurejea nyumbani.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Kata ya Mazimbu, Bahati Mwale, alimshukuru mbunge huyo kwa kutoa misaada mbalimbali katika kata hiyo ikiwamo kuwasaidia wanawake kupata mikopo.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Sheilla Lukuba, alisema lengo la maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ni kutathmini utekelezaji wa afua za kufikia usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi, kijamii na kisiasa katika kufikia maendeleo jumuishi.

Lukuba alisema Halmashauri ya Manispaa hiyo imeendelea kutenga fedha za asilimia 10 katika mapato yake ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mbali na mikopo ya halmashauri, alisema pia kuna Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake wenye masharti nafuu katika mikopo ambao umesaidia kutoa mikopo nafuu na mafunzo ya stadi za biashara kwa wajasiriamali wanawake.

# Wanaume watakiwa kuvunja ukimya manyanyaso

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WANAUME wametakiwa kuvunja ukimya juu ya manyanyaso ambayo wamekuwa wakifanyiwa na wake zao kwa kutoa taarifa kwenye madawati ya jinsia yaliyofunguliwa kwenye vituo vya polisi nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, alisema hayo juzi wakati wa kilele cha Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika kimkoa katika viwanja vya Baraza la Iddi wilayani hapa.

Mndeme alisema mbali na kuwapo kwa taarifa nyingi zinazohusu masuala ya unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto, wako wanaume ambao wamekuwa wakinyanyaswa na wake zao.

Licha ya kuwapo kwa vitendo hivyo, alisema wanaume hao wamekuwa wakiendelea kuvumilia manyanyaso hayo kutokana na kuona aibu.

Akizungumzia juhudi za kumkomboa mwanamke, Mndeme aliwaagiza wakurugenzi wa halmashsuri zote mkoani hapa kupanga asilimia nne ya mapato yao na kutoa mikopo kwa makundi yaliyolengwa kulingana na maelekezo ya serikali ili kuyawezesha kiuchumi.

Mndeme alionyesha kuridhishwa na utoaji wa mkopo kwa makundi hayo katika kipindi cha kuanzia Julai, mwaka jana hadi Februari, mwaka huu.

Takwimu zinaonyesha kuwa Sh. 44,167,441.80 zilitolewa mikopo kwa vikundi 603 vikiwamo 221 vya wanawake katika mkao mzima.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wanufaika wa mikopo hiyo kutoka Wilaya ya Mbinga, Modesta Silomba, Rehema Nkondola na Vereliana Kumburu, waliipongeza serikali kwa kubuni utaratibu huo ambao walidai umewawezesha kumudu kusomesha watoto wao na kuhudumia familia baada ya kikundi chao cha ususi wa masweta, vikapu na kutengeneza batiki kupatiwa mkopo wa Sh. milioni 56.

Akisoma taarifa ya maadhimisho ya siku hiyo, Zuhura Maftari alisema mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia yatasaidia kuiondoa jamii kwenye makundi ya ujane, ugane na watoto yatima.

Wakuu wa Wilaya za Tunduru, Julius Mtatiro, wa Namtumbo, Sofia Kizigo, Cosmas Nsyenye (Mbinga) na Isabela Chilumba (Nyasa), pamoja na mambo mengine, walisema milango ya ofisi zao iko wazi kwa kutoa usaidizi wa kutafuta haki kwa makundi yote.

Mkurugenzi wa shirika lisilo kuwa la kiserikali la usaidizi wa Kisheria la Tunduru Paralegal Centre (TUPACE), John Nginga, alisema yuko tayari kuendelea kutoa elimu katika makundi yote yakiwamo ya wanaume ili kutambua haki zao.



Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango (wa pili kulia), akimkabidhi Katibu Tawala wa Wilaya ya Mtwara, Thomas Salala (katikati), mabati kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Ligula, mkoani Mtwara jana. Kushoto ni Daktari wa Hospitali ya Ligula, Robikieki Kisambu. Benki hiyo, ilikabidhi vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni tano kwa hospitali hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi waelimishwa umuhimu elimu ufundi

**Na Augusta Njoji,** ARUSHA

WAZAZI wametakiwa kuacha tabia ya kuwalazimisha watoto wao kusoma kidato cha tano na sita wanapochaguliwa na serikali kujiunga na vyuo vya ufundi ili wapate ujuzi utakaowasaidia kuajiriwa na kujiajiri.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini humo, Ofisa Udahili wa Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Victor Ngaai, alisema kumekuwa na dhana iliyojengeka kwa baadhi ya wazazi kukataa watoto wao kusoma kwenye vyuo vya ufundi na kutaka kuendelea na masomo ya kidato cha tano na sita jambo ambalo linawanyima uhuru watoto kufikia ndoto zao.

Ngaai alifafanua kuwa serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imekuwa ikiwachagua wanafunzi waliofaulu mtihani wa kidato cha nne wenye ufaulu wa daraja la kwanza na pili kwenye masomo ya Sayansi kujiunga na vyuo vya ufundi ili kuzalisha wataalamu wa fani mbalimbali nchini."Wanafunzi hawa wanaoletwa hapa wamekuwa wakilipiwa na serikali chakula na kukaa bweni bure, na ni waliofaulu masomo ya Sayansi na Hesabu, kuna tatizo pindi mtoto anapochaguliwa kuja chuo, mzazi anakataa anasema anataka akasome kidato cha tano na sita," alisema.

Aliwaasa wazazi kuondokana na dhana kuwa watoto wanaokwenda kwenye vyuo vya ufundi wanapoteza muda na kuwataka kutambua kuwa wanafunzi wanaofaulu vizuri wamekuwa wakijiunga na shahada kwenye fani walizosomea. Alitaja moja ya faida ya wanafunzi kusoma vyuo hivyo ni kujifunza kwa vitendo jambo ambalo linawasaidia kuajiriwa na kujiajiri."Tunahamasisha wazazi waelewe wanafunzi wanapokuja wanajifunza ujuzi na chuo chetu kimebobea kwenye masuala ya teknolojia, na tunazalisha wataalamu kulingana na soko la ajira pia kama vile kwenye tahasusi ya uhandisi wa mabomba, gesi na mafuta hawa wanatengeneza miundombinu ya usafirishaji gesi na mafuta kama mradi wa bomba la mafuta Hoima hadi Tanga," alisema.

Alisema kutokana na azma ya serikali ya kuwa Tanzania ya viwanda na kutekeleza miradi mbalimbali ya mikubwa ya kimkakati pia imekuwa ikiandaa mitaala ili kuzalisha wataalamu kulingana na mahitaji yaliyopo.

"Chuo chetu kinaendana na vipaumbele vya serikali ili kuhakikisha kunakuwapo na wataalamu wa kutosha, tunafundisha pia uhandisi wa umeme na umeme wa nguvu ya maji hapa unaona kabisa wataalamu kwa ajili ya uzalishaji umeme Bwawa la Mwalimu Nyerere tunao," alisema. Naye, mmoja wa wahitimu wa chuo hicho katika uhandisi wa mabomba, gesi na mafuta, ambaye kwa sasa anajitolea kwenye chuo hicho, Glory Kadori, alisema alilazimika kukaa mwaka mmoja nyumbani kabla ya kuanza masomo yake kutokana na wazazi wake kumkatalia kujiunga na chuo hicho wakitaka akasome kidato cha tano na sita.

"Mimi nilichaguliwa na serikali kujiunga na chuo nikitokea Shule ya Wasichana Kifungilo nikiwa na ufaulu mzuri, na nilichagua mwenyewe kuja chuo cha ufundi kutimiza ndoto zangu, lakini ilitokea mvutano nikakaa nyumbani mwaka mmoja na baadaye wazazi walinielewa na kuniruhusu kuja chuo," alisema.

Kwa upande wake, mwanafunzi wa mwaka wa tatu, uhandisi wa mitambo, Fadhil Ringo, aliwaomba wazazi kuacha kuwakatisha tamaa watoto wao wanapochaguliwa kujiunga na vyuo hivyo."Wazazi hawataki kukubali nije kusoma ufundi, lakini mimi nilikuwa naona umuhimu wa kusoma, sio kuja kwenye ufundi unapoteza hapana wala sio ile dhana kwamba ni vilaza, bali ni watu wenye ufaulu mzuri na nilichojifunza naweza kuajiriwa, kujiajiri au kuendelea na shahada," alisema.

HABARI KITAIFA

# Baraza lahamasisha matumizi tiketi mtandao

**Na Gwamaka Alipipi**

BARAZA la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC), limewataka wananchi kuanza kutumia huduma ya tiketi mtandao, kwamba una faida lukuki ikiwamo kuokoa muda na gharama.

Limesema wananchi wanaweza kuipata na kuanza kuitumia huduma hiyo kupitia simu janja, kwa kufanya hivyo itawarahisishia kutunza kumbukumbu.

Rai hiyo ilitolewa jana na Kaimu Katibu Mtendaji wa LATRA CCC, Leo Ngowi, wakati akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kutoa elimu kwa wasafiri katika Kituo cha Mabasi Mbezi Luis.

Ngowi alieleza: "Leo tupo hapa Kituo cha Mabasi Mbezi Luis tukitoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya tiketi za mtandao, tumewafikia wasafiri zaidi ya 50. Wengi wamepakua huduma hiyo kupitia simu janja zao."

Ngowi alisema tiketi mtandao ni mfumo wenye faida nyingi kwa abiria kwani itawaondolea usumbufu wa kufika katika kampuni ya basi husika kukata tiketi, pia itawaokoa na utapeli, ulanguzi wa tiketi unaofanywa na baadhi ya wapigadebe.Alisema ili abiria aweze kukata tiketi yake atalazimika kupakua programu tumishi ya tiketi mtandao katika simu yake kabla ya kuifungua na kufuata maelekezo hadi kwenye malipo.

Aliongeza wataendelea kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi ya mfumo huo mara kwa mara, kwamba mikoani wamejipanga kupitia mabaraza ambayo nayo yatatoa elimu mitaani.

"Hatutaishia leo, kazi hii itakuwa ni endelevu hadi pale jamii kubwa itakapokuwa na uelewa wa mfumo huu. Kama wananchi wanalipia huduma zingine kupitia simu kwa nini washindwe kukata tiketi kwa simu? Elimu zaidi inahitajika," alisema Ngowi.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Kutetea Abiria (CHAKUA), Hassan Mchanjama, alisema: "Tumeupokea vizuri mfumo, ni mfumo mzuri kwa abiria kwani utaondoa ulanguzi pamoja na kupunguza gharama, utawaondolea usumbufu wa kukutana na wapigadebe."

Mfumo wa tiketi za mtandao ulizinduliwa mwaka jana na aliyekuwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, lakini baadhi ya wamiliki wa mabasi wamekuwa wakilalamika kutokana na kuwapo kwa baadhi ya changamoto ambazo zinahitaji kutatuliwa.



Meneja Afya na Usalama wa Kampuni ya Bia ya Serengeti, David Mwakalobo (kulia), akifafanua jambo kwa wanafunzi wa Chuo cha Kilimo cha Wazazi Kaole cha Bagamoyo mkoani Pwani ambao ni wanufaika wa programu ya ufadhili wa masomo inayotolewa na kampuni hiyo inayojulikana kama Kilimo Viwanda, waliotembelea kiwanda cha SBL mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waonywa matumizi ya vibubu kutunzia fedha

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

WANAWAKE wametakiwa kuacha tabia ya kutunza fedha katika vibubu, badala yake wazipeleke katika taasisi za fedha zikiwamo benki.

Imeelezwa kuwa kuhifadhi fedha katika vibubu sio tabia nzuri kwani inaweza kutokea ajali ya moto katika nyumba, hivyo kupoteza fedha zao kwa kuungua tofauti na unavyoweka katika benki.

Hayo yalisemwa juzi na Meneja Biashara wa Benki ya CRDB wilayani Kahama, Dorcas Ngoye, alipozungunza na Nipashe, ikiwa ni sehemu ya kuazimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Ngoye alisema wanawake badala ya kutumia vibubu kuhifadhi fedha, sasa waone umuhimu wa kutumia benki katika kuweka akiba kwa kuwa ni mahali salama kwa fedha zao na wanaweza kuchukua wakati wowote watakapozihitaji.

Alisema vibubu hivyo ni hatari kuweka fedha na pia husababisha matumizi mabaya ya fedha kwa kuwa wakati wowote unaweza kukibomoa na kuchukua fedha, hali ambayo inaweza kuchangia kukaribisha umaskini kwa haraka katika familia.

Meneja huyo wa CRDB alisema katika benki hiyo kuna akaunti ambayo inaitwa 'Malikia' ambayo inaweza kuwasaidia wanawake, na kuongeza kuwa haina makato.

Alisema kuwa benki hiyo imekuwa ikiwasaidia wajasiriamali wadogo katika kuwapa mikopo, huku akiongeza wapo karibu na wanawake katika kutoa elimu ya biashara ili kuona wanasonga mbele katika biashara zao pamoja na kukuza mitaaji walionayo.

Alisema wanawaongezea mitaji wanawake walio katika sekta ya madini kwa lengo la kwenda sambamba na soko la madini, ambalo limekuwa likikua siku hadi siku, hivyo kuliingizia taifa fedha za kigeni.

# Bil. 4.7/- kutatua kero maji Msalala

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 4.7 katika Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, kwa ajili ya kutekeleza miradi mitatu mikubwa ya maji katika kata za Busangi, Segese na Bulyanhulu.

Aidha, zaidi ya wananchi 3,000 wanatarajia kunufaika na miradi hiyo, ambapo miradi ya Busangi-Ntobo na Segese imeshakamilika na wananchi wanaendelea kunufaika na huduma ya majisafi na salama, huku mradi wa Bushing'wa-Bulyanhulu ukiwa katika hatua ya mwisho kukamilika.

Hayo waliyabainisha kwa nyakati tofauti katika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, ya kukagua ujenzi wa miradi mitatu mikubwa ya maji inayoendelea kutekelezwa katika halmashauri hiyo na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), baada ya kupokea Sh. bilioni 4.7 za utekelezaji wa miradi hiyo.

Telack alisema kuwa, serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kitatua kero ya ukosefu wa huduma ya majisafi na salama nchini nzima, hivyo kukabiliana na uhaba ambao ulikuwa ukisababisha kukwamisha shughuli za uzalishaji mali hasa kwa kinamama wanaotumia muda mwingi kutafuta huduma hiyo.

"Ruwasa zingatieni ubora katika ujenzi wa miradi hii, tunataka kuona majisafi na salama yanasambazwa na kuwafikia wananchi katika vijiji vyote vya mkoa huu kwa wakati ifikapo Juni 30 mwaka huu….Tunataka kinamama wa vijijini wafanye shughuli za uzalishaji mali na sio kuchota maji," alisisitiza Telack.

Meneja wa RUWASA mkoani Shinyanga, Mhandisi Julieti Kalovera, alisema upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama vijijini, halmashauri hiyo ni asilimia 65 na wanatarajia kuikamilisha miradi hiyo ifikapo Juni 30, mwaka huu.

# Matatani madai ya dawa za kulevya

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JESHI la Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, linawashikilia vijana wawili, huku likiendelea kuwatafuta mume na mke, kwa tuhuma za kupatikana na kete 439 za dawa za kulevya aina ya heroin katika maeneo ya Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa huo, Ahmed Khamis Makarani, alisema watuhumiwa waliokamatwa ni mtoto wa kike (17), mkazi wa Limbani Wete na Salum Ali (20), mkaazi wa Tumbe ambao walikutwa nje ya nyumba ya watuhumiwa wanaotafutwa, wakiwa na kete 255.

Alisema baada ya kuwakamata watuhumiwa hao, waliingia kwenye nyumba ya watuhumiwa wanaotafutwa ambaye ni Rashid Ali Seif na Zuhura Abdalla Hamad na kufanikiwa kukuta kete 184 kwenye chumba chao cha kulala.

Kamanda Makarani alisema kuwa, walikamata kete hizo katika mkoa jirani wa Kaskazini Pemba kutokana na kuwa wanafanyakazi kwa mashirikiano pale wanapogundua kuna uhalifu, ili kuhakikisha wanatokomeza janga hilo kisiwani Pemba.

# Taulo za kike bado tatizo mahudhurio ya wanafunzi

**Na Halfani Chusi**

TAKRIBANI wanafunzi 1,500 wa kike nchini wanakosa masomo kwa muda wa siku 5-7 kila mwezi, sawa na siku 60-84 kwa mwaka wanapokuwa katika siku zao za hedhi kutokana na kushindwa kumudu gharama za taulo za kike.

Mkurugenzi wa Uhusiano wa Kampuni ya Total Tanzania, Masha Kileo, alibainisha hayo juzi, akinukuu utafiti waliofanya kwa kutembelea familia duni.

Alisema kuwa kwa kutambua hilo, kampuni hiyo kwa kushirikiana na Flavian Matata Foundation, wameamua ndani ya mwezi huu kutoa Sh. moja katika kila lita ya mafuta ili kupata fedha za kuchangia ununuzi wa vifaa hivyo kwa ajili ya kuisaidia wanafunzi wanaotoka katika familia duni.

"Tutatoa shilingi moja katika kila lita moja ya mafuta tutakayouza kwenye sheli zote za Total na baada ya hapo, tutaungana na Flavian Matata katika kununua na kugawa taulo za kike kwa wanafunzi ambao wametoka katika familia duni," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema lengo lao ni kumpatia mtoto wa kike ujasiri wa kujiamini hata wakati akiwa kwenye siku zake ili ahudhurie shuleni wakati wote wa masomo, sawa na ilivyo kwa watoto wa kiume.

"Katika kufanikisha elimu kwa mtoto wa kike, tumeutenga mwezi huu wa Machi kwa kuwa ndiyo mwezi ambao tunaadhimisha siku yetu wanawake," alisema.

Flaviana Matata, mwanzilishi wa taasisi ya kuisaidia watoto wa kike katika nyanja ya elimu, Flaviana Matata Foundation, aliwaomba wadau wengine kujitokeza kufanikisha suala hilo.

"Ninawaomba wadau wanaotumia vyombo vya moto kujaza mafuta katika sheli za Total Tanzania kwa kuwa katika kila lita moja, Total watatoa shilingi moja kwa ajili ya kumchangia mtoto wa kike," alisema na kuongeza kwamba:

"Dhumuni la Flaviana Matata Foundation na Total Tanzania ni kuhakikisha mtoto wa kike habaki nyumbani kwa kukosa taulo za kike pindi anapokuwa katika siku zake."



Mfanyakazi wa kampuni ya mafuta ya Puma Energy Tanzania, Rehema Migambile, akijaza mafuta bure kwenye gari la mwanamuziki, Judith Wambura a.k.a Lady J Dee (wa tatu kushoto), katika kituo cha Puma cha Upanga, jijini Dar es Salaam juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: JOHN BADI**

# Mama lishe watakiwa kuthaminiwa

**Na Devota Mwachang'a**

MWANAHARAKATI wa Utetezi Wanawake na Watoto ametoa wito kwa jamii kuwathamini na kuutambua umuhimu wa wanawake wauza vyakula maarufu kama 'Mama Lishe' kwa kuwa wana nafasi katika kuwalea 'wasimbe' na 'makayanda' nchini.

Msimbe ni mwanamke aliyefikia umri wa kuolewa, lakini hajaolewa, na Kayanda ni mwanaume aliyefikia umri wa kuoa na hajaoa maarufu kama 'mabachela'.

Hayo yamebainishwa katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, kwa Mwanaharakati anayetetea haki za wanawake na watoto, Latifa Masasi, kuandaa Tamasha la Mama Lishe lililowaakutanisha pamoja na wanaume 'Baba bora', watoto yatima na wadau wengine.

Akizungumza katika tamasha hilo lililofanyika viwanja vya Mwembeyanga, Temeke juzi, Masasi alisema mama lishe wakithaminiwa wanaweza kujiamini na kufanya biashara yao vizuri, kujipatia kipato kitakachowawezesha kulea familia zao bila hofu.

"Lazima tuitambue thamani ya mama lishe ninawakusanya katika umoja wao na kuwasaidia kwa kuwapatia mahitaji mbalimbali kwa kadri ninavyojaaliwa ili kuhakikisha hawatetereki wanajikwamua na kuhudumia jamii," alisema.

Masasi amebainisha kuwa bila kujali umuhimu watoa huduma hao, wapo wateja wakorofi ambao badala ya kulipia chakula wanachopewa wao wanakuwa kero kwa Mama Lishe na kuwanyanyasa, wanapodai haki zao.

Ofisa Afya Temeke, Rehema Sadick, alisema kuwa Mama Lishe ni muhimu katika jamii, chakula kwa watu wengi katika maeneo mbalimbali hasa wa kipato cha chini ambao ni wengi kwa asilimia kulinganisha na wa kipato cha kati na cha juu wanaokula kwenye hoteli kubwa nchini.

"Mama Lishe wanastahili waangaliwe, wawezeshwe, ili watoe huduma bora ya chakula salama inayozingatia na kulinda afya ya walaji wa vyakula wanavyoviandaa," alisema.

Mmoja wa Mama Lishe, Vick Msemo, akiwawakilisha mama na baba lishe wa Soko la Tandika, ameomba uongozi wa Manispaa ya Temeke uwajengee banda imara na miundombinu bora itakayowezesha Mama na Baba lishe kati ya 40 na 50 kufanyabiashara yao kwa uhuru na usalama.

Hamis Mbwana, amekiri uwapo wa usumbufu unaofanywa na baadhi ya wanaume dhidi ya mama lishe hasa baada ya kushiba.

# H/shauri zaagizwa maeneo uwekezaji

**Na Vincent Tiganya,** TABORA

HALMASHAURI mkoani Tabora zimeagizwa kupima na kutenga maeneo ya uwekezaji ili kuhamasisha na kuvutia wawekezaji toka ndani na nje ya nchi.

Maagizo hayo yalitolewa na Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Philemon Sengati, alipokuwa akifungua kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

Alisema maeneo hayo yatolewa kwa wawekezaji bila malipo na visiwapo vipingamizi visivyokuwa na msingi wakati wa utoaji maeneo kwao ili Mkoa upate viwanda vingi.

"Tunataka tuwatengenezee wawekezaji mazingira mazuri waje kwa wingi, tunataka tuwe na viwanda vikubwa ambavyo vitasaidia kuinua mkoa wetu na kutoa ajira kwa vijana wetu… katika hili lazima tuwe na mtazamo wa pamoja kama Mkoa wa kuvutia wawekezaji wengi," alisisitiza.

# Mbunge achangia ujenzi sekondari

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

MBUNGE wa Jimbo la Bunda Mjini, Robert Chacha Maboto, ameeleza kufurahishwa na wakazi wa Kata ya Nyamakokoto katika Halmashauri ya Mji wa Bunda, ambao wameamua kujenga sekondari kwa kutumia nguvu zao.

Lengo ni kuwanusuru wanafunzi wanaotembea umbali mrefu kwa ajili ya kutafuta elimu, waweze kusoma kwa ukaribu zaidi na kutokukatisha masomo yao.

Kutokana na hali hiyo, amechangia shilingi milioni mbili taslimu katika ujenzi wa shule hiyo mpya, ambapo Halmashauri ya Mji wa Bunda sasa itakuwa na shule za sekondari mpya sita.

Akikabidhi mchango huo juzi kwa uongozi wa kata hiyo kwa niaba ya mbunge huyo, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Michael Kweka, alisema mbunge huyo alivutiwa na wazo la wananchi wa Kata ya Nyamakoko, kwa kuamua kuanza ujenzi wa shule ya sekondari katika kata hiyo.

Mwenyekiti huyo alisema kwamba mbunge ameamua kuchangia shilingi milioni mbili ili kuunga mkono nguvu za wananchi wake.

Kweka alisema kuwa mbunge huyo ameahidi kuendelea kuchangia zaidi katika shughuli mbalimbali za maendeleo katika jimbo hilo na wilaya nzima kwa ujumla.



JUKWAA LA UONGOZI

**Suu Kyi: Mwanamama mshindi wa tuzo Nobel na mzoefu wa kizuizini**

Ukurasa 14



Ukurasa 13

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

**Wakumbushana harakati zianzie familia, kisha kupanda ngazi siasa**


# siasa

JUMATANO MACHI 10, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


# Mgongano kifamilia, mtoto na wajukuu wa Mfalme Uingereza

• Bibi Eliza hana tabu, shida kuu...; 'Watoswa', wafadhiliwa Marekani



Mwanamfalme Harry, akiwa na mkewe Meghan Markle. **PICHA: MTANDAO**

MEGHAN Markle, mke wa mwanamfalme Harry na mkwe wa Malkia, amesema kuna wakati maisha yalimbana na kuwa magumu sana katika familia ya kifalme na 'hakutaka tena kuwa hai' akisema kwamba hakupata msaada hata alipouomba.

Anasema kibaya zaidi ilikuwa wakati mtu mmoja wa familia hiyo alipomuuliza Harry jinsi mtoto watakayemzaa atakuwa na 'ngozi nyeusi.'

Prince Harry, pia alifichua kwamba baba yake Prince Charles, aliacha kuzipokea simu zake, alipogundua kwamba alikuwa na mpango wa kujiondoa kutoka familia ya kifalme.

Wawili hao wamezungumzia masuala mbalimbali ikiwamo ubaguzi wa rangi, uhusiano wao na vyombo vya habari, afya ya akili na mambo katika familia ya kifalme.

Pia walitangaza kwamba mtoto wanayemtarajia hivi karibuni atakuwa msichana.

Wawili hao walihamia Carlifornia baada ya kujitoa kutoka majukumu ya familia ya kifalme Machi 2020 na ilitangazwa mwezi uliopita kwamba hawatarejea kama wanachama wa familia ya kifalme.

Meghan anasema, alianza kuhisi upweke wakati vikwazo vilipowekwa kuhusu aliyoweza kufanya, akifichua kwamba wakati mmoja hakuweza hata kuondoka nyumbani kwa miezi kadhaa.

Anapoulizwa iwapo aliwahi kufikiria kuhusu kujidhuru au kuwa na mawazo kama hayo alijibu "Ndio...hilo lilikuwa bayana sana, wazi sana na la kuogofya, sikujua ningemwendea nani."

Meghan anasema, alihisi kuzongwa na picha ya hafla rasmi waliokuwa wamehudhuria na Harry katika ukumbi wa Royal Albert Hall, Uingereza alipokuwa mjamzito.

"Mwanzoni tulilazimika kwenda katika hafla hiyo nilikuwa nimezungumza na Harry kuhusu suala hilo asubuhi hiyo," Meghan anasema na kuongeza alihudhuria hafla hiyo na Harry usiku huo kwa sababu alihisi hakutaka kusalia mpweke na alikumbuka Harry akimshika mkono wakiwa katika hafla hiyo.

Kuna madai familia ya kifalme ilishtumiwa kwa kushindwa kumliwaza, Harry na Mkewe huku Meghan akisema hali 'ilianza kuwa mbaya ' baada ya wao kuoana Mei, 2018.

"Familia ya ufalme ilikuwa na wasiwasi kuhusu ngozi ya mwanangu. Niligundua kwamba sikuwa tu nikilindwa, pia walikuwa tayari kusema uongo, ili kuwakinga baadhi ya watu wa familia ya kifalme," anasema.

"Lakini hawakuwa tayari kusema ukweli kunilinda pamoja na mume wangu," anasema Meghan.

INAENDELEA UK.12

UCHAMBUZI

# Mgongano kifamilia, mtoto na wajukuu wa Mfalme Uingereza

INATOKA UK.11

Kuhusu uvumi kwamba alimfanya mke wa kaka yake Catherine kulia kuhusu tofauti waliokuwa nayo kuhusu marinda yenye maua, alidai ni habari zilizosababisha taarifa nyingi za uvumi kuchapishwa.

Meghan anasema ni kinyume na kilichofanyika na Catherine baadaye aliomba msamaha na kumletea maua na kijikaratasi chenye maandishi ya kuomba radhi.

Akiungana na mkewe, Harry alizungumzia uhusiano wake na watu wengine wa familia ya kifalme akiwamo bibi yake Malkia ulikuwa mzuri sana na wawili hao huzungumza kila mara.

Hata hivyo anasema uhusiano kati yake na baba yake mwanamfalme Charles wa Wales, umevurugika na Harry anasema anahisi kuangushwa an mzazi wake huyo. Aliongeza kwamba ataendelea kumpenda lakini kuna nachokiita, kuumizwa kwingi' kulikotokea' kumhusu Mwanamfalme William na 'wapo katika njia tofauti.'

Pia alifichua kwamba familia yake ilikuwa imekoma kumpa msaada wa kifedha.

**ANAYEWAFADHILI LEO?**

Harry na Meghan baada ya kusitishwa kwa ufadhili wao na Familia ya Kifalme - tajiri wa Marekani Tyler Perry ndiye aliyewapa hifadhi ya makao na ulinzi katika eneo la California mwaka 2020.

Huyo ni mtengenezaji filamu mashuhuri, mchekeshaji, mwigizaji, mzalishaji wa vipindi na mtunzi, ambaye filamu zake na vipindi vya kwenye televisheni, ndio chanzo kinachomfanya kuwa mmiliki wa nyumba Marekani, kutoka kundi la Wamarekani weusi.

Perry anafahamika sana kwa filamu zake za Madea alizoandika, akazisimamia, mwelekezi na aliyeshiriki kama mhusika mkuu kuhusu mwanamke mzee anayeetumia viungo bandia.

Mwaka 2015, alijenga studio yake ndani ya eneo kubwa analomiliki, nje ya eneo la Atlanta, Georgia na mwaka jana ndio alitambuliwa kuwa bilionea, kwa mujibu wa jarida la Forbes.

Katika upande wa pili, pia anagonga vichwa vya habari, pale alipoweka wazi kwamba anapitia magumu katika maisha, hasa mkasa kuachana na mchumba wake wa muda mrefu, na mama wa mtoto wake mmoja, Gelila Bekele.

"Nina miaka 51, sina mchumba na najiuliza ukurasa wangu wa maisha unaofuata utakuwaje? Haijalishi vile hali itakavyokuwa, nitasimama na Mungu, nitakuwa baba mzuri kadiri ya uwezo wangu, na kujitahidi kwa kila namna," aliandika Perry, katika ukurasa wake wa Instagram.

"Katika dunia yenye huzuni nyingi, tafadhali jitahidi kuwa mzuri!" anasema na katika maandishi yake hayo ya mtandao, aliandika sababu za uamuzi wake kuishi na wanandoa hao katika moja ya majumba yake ya kifahari .



Mwanamfalme Harry, mkewe Meghan Markle na mtoto wao. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Ni kinyume na kilichofanyika na Catherine baadaye aliomba msamaha na kumletea maua...



Bibi Malkia Elizabeth wa Uingereza.

Anasema, alitumia ulinzi wake walipokuwa wanahama kutoka Canada hadi Los Angeles, Marekani mwaka jana.

Mwanamfalme Harry na Meghan, wanasema uaamuzi wao kuondoka baada ya eneo la nyumba waliokuwa wanaishi katika kisiwa cha Vancouver, Magharibi mwa Canada, kufahamika na watu wengi.

"Hatukuwa na mpango wowote," Meghan anasema katika mazungumzin na wanahabari, akiongeza: "Tulihitaji nyumba na (Tyler Perry) alijitolea kutusaidia na maofisa wake wa ulinzi, pia na hilo likatupatia fursa ya kupumua na kufikiria hatua tutakayochukua."

Tyler Perry hajatoa tamko lake kwanini aliamua kumsaidia Meghan na Harry. Mwanamfalme huyo anatamka: "Wasiwasi mkubwa ulikuwa ni kwamba wakati tuko Canada, katika nyumba ya mtu mwingine, niliarifiwa kwamba ulinzi utaondolewa ndani ya kipindi kifupi."

Harry ana ufafanuzi: "Ghafla ikanijia akilini kwamba, nikkafikiria kwa haraka mipaka inaweza kufungwa, ulinzi wetu utaondolewa na hakuna anayejua hatua ya kufungiwa itaendelea kwa muda gani. Dunia inajua tuko wapi, sio salama na bila shaka tutahitajika kuondoka hapa.'"

Wanandoa hao wanaasema, kwamba baadaye, waliamua kwenda kuishi California na kununua nyumba iliyoko Montecito.

**SAFARI WALIKOTOKA**

Prince Harry katika mazungumzo yake na televisheni moja, alishatamka kuwa mengi yanayochapishwa katika magazeti ya udaku siyo ya kweli, akisisitiza kwa kauli "sitakubali kuingizwa katika hujuma iliyomuua mama yangu."

Harry anasema kumbukumbu ya kifo cha Princess Diana ilikuwa bado ingalipo kila siku kunavyokucha na sio kwamba yeye mwenye amejawa na hofu.

Mkewe wa sasa na nyota wa zamani wa televisheni ya Marekani, Meghan Markle, anasema wakati marafiki zake wa Uingereza walikuwa na furaha yeye kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Harry, walimuonya wasioane kwa sababu magazeti ya udaku ya Uingereza yangewaharibia.

Kuhusu namna anavyoweza kukabiliana na ufuatiliaji mzito wa magazeti hayo, Meghan anaeleza: "Ukweli ni kuwa nimekuwa kwa muda mrefu nikimwambia 'H' - hivyo ndivyo ninavyomwita. Haitoshi kuwa utanusurika katika jambo, hiyo siyo maana ya maisha. Inatakiwa upate mafanikio."

Baada ya ndoa yao, walifungua mashtaka dhidi ya gazeti la udaku la Uingereza 'The Mail on

INAENDELEA UK.14

SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

# Wakumbushana harakati zianzie familia, kisha kupanda ngazi siasa

Na Sabato Kasika

"WANAWAKE Katika Uongozi Chachu Kufikia Dunia Yenye Usawa," ni kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mwaka huu, ikilenga kuhimiza usawa wa kijinsia.

Ni mtazamo unaozaliwa katika kudai usawa wa kijinsia, ambayo ni moja ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa, hivyo unatiliwa mkazo, kwa kuwa unafanikishwa kupitia utendaji wa haki kati ya wanaume na wanawake.

Siku ya Wanawake Duniani iko kila Machi 8 ya mwaka, ikilenga kutathmini utekelezaji afya zikifikiwa katika mtazamo wa usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, kijamii, kisiasa kufikia maendeleo jumuishi.

Ni tukio linalotoa fursa ya kuelimisha jamii kuhusu jitihada zilizofanywa na jamii, serikali, asasi za kiraia, sekta binafsi na wadau wengine kukuza hali ya mwanamke wa Kitanzania.

Aidha, ni ukumbi mwingine unaowapa wadau hao fursa ya kubainisha upungufu na mbinu za utatuzi wa changamoto zinazowakabili wanawake.



Mkurugenzi wa taasisi ya WAJIKI, Janeth Mawinza. **PICHA: MTANDAO**

### WENYE SIKU YAO

Justa Mwaituka, ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kota Women Health and Development (KIWOHEDE), anayesema uongozi kwamba suala la uongozi si la siasa pekee, bali inaanzia kwenye familia na jamii, ikilenga kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo yao, kwa kuwa dhana ya uongozi ipo katika nyanja zote.

"Kwa hiyo, ili kufikia usawa wa kijinsia katika uongozi, kuna haja ya kuandaa miundombinu mbalimbali, yakiwamo mafunzo kwa wanawake na hasa wa vijijini ili kujua haki zao," anasema Justa.

Pia ana ufafanuzi kwamba hayo yanapaswa yafanyike kuanzia vijijini, kwenye halmashauri, mikoa na taifa ili kushawishi wanawake wengi zaidi kutambua kuwa wanapaswa kujua wajibu wao kuanzia familia, hadi penye tafsiri pana kwa ujumla.

"Nikumbushe kuwa duniani kote haijawahi kutokea ikawapo '50 kwa 50' katika uongozi, hivyo ni muhimu wanawake kuelekeza nguvu katika kutafuta uongozi wa ngazi ya familia badala ya kufikiria siasa tu," anasema, huku akitaja haja ya kuwapo dira ya kufikiwa hatua kubwa, kuliko ilivyo sasa.

"Pamoja na kwamba mapambano ya kutafuta usawa wa kijinsia ni muhimu, lakini tusiegemee kwenye siasa, bali tujikite zaidi kutafuta uongozi kuanzia ngazi ya familia kwanza ili kuondoa mfumo dume," anaongeza.



Mkurugenzi Mtendaji wa KIWOHEDE, Justa Mwaituka.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza, anasema kufikia usawa wa kijinsia katika uongozi, ndilo lengo la wanawake, lakini bado kuna safari ndefu.

"Wanawake wengi wanatamani kuwania nafasi za uongozi katika kata na majimbo, lakini bado wanaachwa nyuma na kujikuta wanakiwa wa viti maalum tu huku wakichaguliwa wachache," anasema Janeth.

Anatoa mfano kwamba katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana, wanawake waliochaguliwa katika kata na majimbo ni wachache kuliko wanaume, hali inayomfanya aamini kuwapo safari ndefu kufikia dhana na lengo la '50 kwa 50.'

"Viongozi mbalimbali wakiwamo wa vyama vya siasa watafakari kwa kina katika maadhimisho ya siku hii na kuangalia uwezekano wa kuwapa kipaumbele wanawake katika nafasi za juu za uongozi," anasema.

Anasisitiza rai kwamba umefika wakati sasa wa nafasi za uongozi ukiwamo wa kisiasa, kuwa na mrengo wa kijinsia badala ya kusemwa tu pasipo utekelezaji, huku wanawake wakiendelea kuwa wa viti maalum katika siasa.

"Mkoa ukiwa na majimbo 10, yagawanywe matano, kwa ajili ya wanawake na matano mengine kwa ajili ya wanaume, hapo kutakuwa na mrengo wa kijinsia, lakini vinginevyo, wanawake wataendelea kubaki nyuma," anasema.

> "Viongozi mbalimbali wakiwamo wa vyama vya siasa watafakari kwa kina katika maadhimisho ya siku hii na kuangalia uwezekano wa kuwapa kipaumbele wanawake katika nafasi za juu za uongozi.

### HALI ILIVYO

Katika maadhimisho ya mwaka jana, ilielezwa kuwa katika miaka ya 1990 na kabla ya hapo, kinamama walikuwa wanafanya kazi nyingi na kupata ujira kidogo, walinyanyaswa na hawakupewa kipaumbele, ikilinganishwa na wafanyakazi wenzao wanaume.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika Wizara ya Afya, Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Prudence Constantine, anafafanua serikali imeendelea na jitihada za kuwawezesha kinamama kiuchumi, kwa kuwaanzishia mifuko ya uwezeshaji kiuchumi.

Anaziorodhesha kuwa ni pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, wenye masharti nafuu ambao umewasaidia kutoa mikopo nafuu na mafunzo ya stadi za biashara kwa wajasiriamali wanawake.

Kwa mujibu wa msemaji huyo, tangu mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2018/19, serikali ilishatoa fedha Sh. bilioni 28.8 zilizosaidia vikundi vya wanawake 13,691 na kufanya idadi ya walionufaika na fedha hizo kufikia 883,724 ikilinganishwa na wanawake 12,842 kwa mwaka 2013/14.

Mtazamo wa kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka jana ni 'Kizazi cha Usawa kwa Maendeleo ya Tanzania ya Sasa na Baadaye' iliyosisitiza kuelimisha jamii umuhimu wa kuwapo usawa wa kijinsia kufikia malengo ya maendeleo endelevu.

JUKWAA LA UONGOZI

# Suu Kyi: Mwanamama mshindi wa tuzo Nobel na mzoefu wa kizuizini

• Binti pekee wa Jenerali aliyepigania uhuru



Aung San Suu Kyi, alipokutana na Rais Barack Obama. **PICHA: MTANDAO**

**Na Christina Mwakangale**

AUNG San Suu Kyi, ni kati ya wanawake maarufu duniani wanaopambania demokrasia katika kutetea haki za binadamu.

Licha ya kukumbana na magumu kadhaa ikiwamo kuwekwa kizuizini, mshindi huyo wa Tuzo ya Amani ya Nobel mwaka 1991, ameendelea kubakia kwenye siasa takribani miongo minne, akipata na misukosuko tele.

Suu Kyi (75), mtoto pekee wa kike wa mpigania uhuru wa nchi hiyo, Jenerali Aung Sun, aliyeuawa wakati babaye Kyi, akiwa na miaka miwili.

Mapema Februari mwaka huu, Jeshi la Myanmar lilifanya mapinduzi ya kijeshi na kuchukua madaraka, huku likitangaza hali ya tahadhari kwa nchi kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Suu Kyi, kiongozi wa Chama cha National League for Democracy (NLD) kilichopo madarakani, alikamatwa pamoja na wanasiasa wengine mapema siku hiyo hiyo ya mapinduzi.

Mama huyo alishawekwa kuzizini kwa vipindi tofauti, ikiwamo mwaka 1990, 2000 na hivi sasa.

> Baada ya kumkamata kiongozi wa NLD, televisheni ya nchi hiyo ilitangaza kuwa taifa lipo kwenye hali ya dharura kwa muda wa mwaka mmoja.

Harakati zake, ni tangu kupata msukumo na hamasa kwa wanaharakati waliomtangulia, wakiwamo Martin Luther King wa Marekani na Mahatma Gandhi wa India.

Mwaka 1988, jeshi la nchi yake lilichukua utawala kupitia mapinduzi Septemba na serikali ya kijeshi iliitisha uchaguzi mwezi Mei, mwaka 1990 na Chama cha Suu Kyi kushinda kwa kura nyingi, licha ya kukataliwa kupewa madaraka.

Ni kipindi hicho ndio, Suu Kyi, aliwekwa kifungoni nyumbani eneo la Yangon kwa muda wa miaka sita, hadi alipoachiliwa mnamo Julai, mwaka 1995.

Aliwekwa tena chini kifungoni nyumbani Septemba mwaka 2000 na baada ya miaka mwili ya kifungo cha nyumbani, alifunguliwa mashtaka. Alidumu nyumbani hadi mwaka 2010, alipokamatwa wakati akisafiri kuelekea mjini Mandalay, kutokana na kukiuka masharti ya kutosafiri.

Mwaka 2015 alikiongoza chama chake katika uchaguzi wa kwanza wa wazi tangu miaka 25 ipite na kilipata ushindi, ila alikataliwa kushika nafasi hiyo kutokana na sababu kwamba ana watoto ambao si wa taifa la Myanmar.

Hadi mapinduzi yalipofayika mapema Februari, mwaka huu, Suu Kyi alitambulika kama Mshauri wa Serikali.

**SAFARI YA NYUMBANI**

Mwaka 1960 alielekea India na mama yake Daw Khin Kyi, ambaye alikuwa ameteuliwa kuwa Balozi wa Myanmar mjini Delhi na miaka minne baadaye, alienda masomoni katika Chuo Kikuu cha Oxford nchini Uingereza, alikosomea filosofia, siasa na uchumi. Huko ndiko alikokutana na mumewe, msomi Michael Aris.

Baada ya kuishi na kufanya kazi nchini Japan na Bhutan, aliienda Uingereza ambako alikuwa akiwalea wanawe wawili, Alexander na Kim, lakini Maynmar haikuwa mbali na fikra zake.

**MAPINDUZI YALIYOJIRI**

Jeshi la Myanmar mapema mwaka huu, lilithibitisha kulidhibiti taifa hilo baada ya kumweka kizuizini kiongozi wa taifa hilo, Aung San Suu Kyi.

Baada ya kumkamata kiongozi wa NLD, televisheni ya nchi hiyo ilitangaza kuwa taifa lipo kwenye hali ya dharura kwa muda wa mwaka mmoja.

Mkutano wa Kwanza wa Baraza jipya la Mawaziri, ulifanyika baada ya mapinduzi ya kijeshi ya Februari Mosi, baada ya mijadala kuhusu udanganyifu katika uchaguzi mkuu uliofanyika Novemba 8, mwaka jana.

Idara ya Mawasiliano ya Jeshi la Myanmar, ilisema mkutano wa Baraza la Mawaziri ulifanyika Ikulu ya Rais pamoja na Mkuu wa Wafanyakazi wa Umma na Rais Min Aung Hlaing, Naibu Mwenyekiti, Myint Swe na wajumbe tisa wa baraza waliochukua nafasi za mawaziri waliofutwa kazi.

Ilibainika katika mkutano huo kwamba, Rais Hlaing alijadili mpango wa utekelezaji majukumu ya mawaziri katika kipindi cha hali ya dharura ambayo itadumu kwa mwaka mmoja.

Iliripotiwa kuwa masuala kama vile kuendelea kwa safari za ndani na utalii, kufungua mahekalu na sehemu za ibada, kuendelea na shughuli za sekta za uchumi kulingana na hatua za Covid-19, kufufua uchumi na kuongeza fursa za kazi pia zilijadiliwa katika mkutano huo.

Polisi nchini Myanmar limemfungulia mashtaka Suu Kyi, baada ya kumkuta na simu za upepo nyumbani kwake, ikielezwa simu hizo zilikutwa nyumbani kwake bila ya kusajiliwa. Mashtaka hayo yanaonyesha, ikithibitika anakabiliwa na kifungo cha hadi miaka miwili jela.

Nyaraka za mashtaka zinaonyesha, simu hizo zilikuwa ni kwa ajili ya kutumiwa na walinzi wake.

Myanmara ambayo kwa sasa inaongozwa na Mkuu wa Majeshi, Jenerali Min Aung Hlaing, tangu mapinduzi hayo ya maandamano yameongezekana watu wanaendelea kuingia mitaani katika mji mkubwa.

Myanmar ni nchi ya Asia ya Kusini Mashariki, inayojulikana pia kwa jina la Burma au Baman na wamepakana na China upande wa Kaskazini, Laos upande wa Mashariki, Uthai Kusini - Mashariki na Bangladesh upande wa Magharibi.

Nchi hiyo imepakana na Bahari Hindi kwa urefu wa kilomita 2,000 wakiwa na jumla ya makabila takribani 135 wazungumzao lugha kadhaa, theluthi mbili ni jamii ya kutoka Milima ya Tibet wanakotokea mababu zao zaidi ya miaka 1000 iliyopita.

## Mgongano kifamilia, mtoto na wajukuu wa Mfalme Uingereza

**INATOKA UK.12**

Sunday' kwa kuingilia maisha yao ya faragha, akidai ni kinyume cha sheria. Walichapisha barua aliyomwandikia baba yake.

**OBAMA ATETA NAYE**

Mwaka 2017, Rais wa Marekani wakati huo, Barack Obama, alimwambia Prince Harry wa Uingereza kwamba: "Kwenye mitandao ya jamii kuna hatari moja ya watu kuwa na ufahamu tofauti juu ya uhakika wa mambo na kuzama katika taarifa ambazo zinashinikiza kuendelea kushikilia maoni potofu."

Harry alimhoji Obama mnamo Septemba 2017, ambayo ilitolewa kwenye vyombo vya habari , Rais Obama, akifafanua kwamba ni muhimu kwa wanaotumia mitandao wakatafuta njia ya kuwasiliana ana kwa ana, ili wafahamiane.

"Kwenye mitandao kila kitu kinapambwa na unapokutana na watu ana kwa ana unagundua kuwa watu wana matatizo yao," Obama anasema.

"Pia utagundua mambo yanayowaunganisha watu kwa sababu unashuhudia kuwa mambo siyo mepesi hivyo kama yanavyoonyeshwa katika kumbi za mitandaoni," anaongeza.

Kwa mujibu wa Obama, watu wanapokutana kwa uso, inakuwa ngumu kwao kuonyeshana chuki na ukatili, kama ilivyo katika hali ya mitandao.

**Kwa mujibu wa taarifa za BBC, VOA na mtandao**





# Wigo mikopo elimu ya juu waongezeka

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

SERIKALI imesema imeongeza wigo wa idadi ya wanafunzi wa mikopo ya elimu ya juu kutoka wanafunzi 125,126 mwaka 2015 hadi kufikia 142,179 mwaka 2021.

Hayo yalibainihwa na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema kutokana na jitihada za serikali kuwekeza katika sekta ya elimu imekuwa na mchango mkubwa wa kuongezeka kwa idadi hiyo kwa kipindi cha miaka sita.

Pia alisema katika kipindi hicho cha miaka sita kiwango cha mikopo kimeongezeka kutoka Sh. bilioni 341 mwaka 2014/15 hadi kufikia Sh. bilioni 462 mwaka 2020/21.

"Jumla ya fedha iliyotumika kwa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kuanzia mwaka 2015 hadi 2021 ni Sh. trilioni 2.82.

Kadhalika, alisema kuwa kwa kutumia mifumo ya kielektroniki kumeongeza ufanisi wa utendaji, kwani sasa hakuna ucheleweshaji wa mikopo ya wanafunzi labda kuwe na sababu nyingine za mtu mmoja mmoja.

"Katika sekta ya elimu, nchi yetu ni kubwa na kazi zinaendelea kwa kasi napongeza wizara zote mbili Elimu na TAMISEMI na taasisi zao kwa usimamizi huu nawatia moyo kazi iendelee," alisema Dk. Abbasi.

Alisema, serikali itaendelea kutoa fedha za elimu msingi bila ada kila mwezi, itaendelea kuajiri walimu, kusambaza vifaa na kuanza kutekeleza miradi mbalimbali na wabia ukiwamo ule wa Benki ya Dunia wa zaidi ya Sh. trilioni 1 ambazo matayarisho ya utekelezaji yanakwenda vizuri.

"Aidha, kama mnavyofahamu kazi ya kuandaa mihutasari kwa ajili ya somo la Historia ya Tanzania imekamilika kwa somo la kuanzia awali hadi kidato cha sita.

"Mwelekeo sasa ni kukamilisha taratibu nyingine somo hilo lianze kufundishwa kwa kina zaidi Julai, 2021," alisema.

Vile vile, alisema kuwa katika kipindi hicho serikali imeboresha miundombinu mbalimbali ya elimu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa hadi kufikia 125,215 mwaka 2021.

"Zaidi ya nyumba za walimu 1,780 zimejengwa, ukarabati mkubwa wa miundombinu katika shule kongwe, sekondari 86 kati ya 89 kongwe ujenzi umekamilika ikiwamo kuijenga upya Sekondari ya Ihungo, Kagera," alisema.

Pia alisema ujenzi wa maabara katika shule za sekondari 1,696 kwa ajili ya masomo ya sayansi zimejengwa, magari 26 ya Maafisa Elimu Mikoa, magari mengine 184 yamenunuliwa kwa kazi ya ufuatiliaji wa elimu na pikipiki 3,909 zimetolewa kwa Maofisa Elimu Kata.

Hata hivyo, alisema jumla ya walimu 26,181 wa shule za msingi na sekondari na mafundi sanifu wa maabara za sekondari 397 wameajiriwa.

# Wanawake 'waamshwa' vita dhidi ya ukatili

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WANAWAKE wametakiwa kuwa mstari wa mbele kupiga vita vitendo vya ukeketaji, mimba za utotoni na ndoa ambazo zimekuwa tatizo sugu kwa jamii, ili kupunguza ukatili wa kijinsia unaoendelea nchini.

Hayo yalibainishwa na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma, Fatma Toufiq, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.

Toufiq alisema suala la ukeketaji kwa wanawake imekuwa tatizo kubwa na lina unyanyasaji ndani yake, hivyo wanawake ambao ni jeshi

kubwa wanapaswa kuwa mstari wa mbele kulikemea ili kuhakikisha linatoweka kabisa.

Alisema pale wanapoona kuna tatizo hilo wanapaswa kutoa taarifa na ushirikiano wa kuhakikisha mhusika anayetenda vitendo hivyo anachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Naomba sisi wanawake wenyewe tuwe walinzi katika suala la ukeketaji kwa wanawake na watoto, kwa sababu linamnyanyasa mwanamke na haikubaliki kisheria," alisema Toufiq.

Akizungumzia mimba na ndoa za utotoni, alisema tatizo hilo linachangia kwa kiasi kikubwa kukatisha ndoto za watoto wa kike kutokana na kuwa wanaozeshwa mapema na kuwakatisha masomo yao.

Mbunge huyo alisema wanawake wanapoona kuna vitendo hivyo, wanapaswa kuvikemea ili kuwasaidia watoto wa kike waweze kuendelea na masomo na kutimiza ndoto zao za baadaye.

Aliwahamasisha wanawake kuendelea kujitokeza kwa wingi kushiriki katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo ikiwamo kugombea

nafasi za uongozi, kwani wamekuwa na mchango mkubwa katika kuongoza jamii kupitia idara na vitengo mbalimbali ambavyo wanavihudumia.

Kwa upande wa Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalang'anya, alisema hali ya wanawake

kujitokeza na kusema ukweli juu ya yale wanayofanyiwa kumewafanya wanaume kutambua kuwa mwanamke sio watu duni wala si wa kudhalilishwa bali wanapaswa kupewa nafasi.

Nabalang'anya alisema mwanamke uwezo wake katika kuamua mambo mbalimbali kuanzia kwenye ngazi ya familia, unampa ujasiri wa kufanya maamuzi mazuri anapokuwa katika nafasi ya uongozi.



Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna (kulia), akizungumza na viongozi wa soko la mboga na matunda la Makole jijini jana, kuhusu utii wa sheria na kanuni za masoko kwa wafanyabiashara wote. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# UWK: Matapeli tiba asili wapuuzwe

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

MAKAMU Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Kikristo Dodoma (UWK), Grace Makata, amewataka wanawake kutokukurupuka na matangazo yanayotolewa na waganga wa tiba asili, kujinadi kuwa wana uwezo wa kutibu ugonjwa wa Covid-19 kwa kuwa wengine ni matapeli.

Aidha, amewataka wanawake hao badala ya kukurupuka kwenye tiba hizo za asili ambazo hazina viwango vilivyothibitishwa na wataalamu na Mkemia Mkuu wa Serikali watumie muda huo kumuomba Mungu.

Makata alisema hayo alipokuwa akizungumza na wanawake kwenye ibada ya maombi ya Siku ya Wanawake Duniani iliyofanyika Kanisa Kuu la Anglikana Dayosisi ya Central Tanganyika.

Alisema hivi sasa kutokana na janga la ugonjwa wa corona, kuna baadhi ya waganga wa tiba za asili wanajitokeza kwa kupitia matangazo yao kuwa wana uwezo wa kutibu ugonjwa huo wakati siyo kweli.

Alisema kutokana na hali hiyo, wanawake wanatakiwa kutokukurupuka na matangazo hayo, ambayo hayana hata kibali kutoka kwa wataalamu wa afya, ikiwamo Mkemia Mkuu wa Serikali.

"Kipindi hiki cha janga hili la Covid -19, tunatakiwa kumtanguliza Mungu wetu mbele kwa kuomba na kufunga, kwa kuwa yeye ndiye atakayetuponya na siyo hizo dawa za asili ambazo ni za kitapeli," alisema.

Akizungumza kwenye maombi hayo ambayo yaliambatana na kumwomba Mungu ili corona itoweke, aliwataka wanawake kuhakikisha wanamtumikia Mungu kwa uaminifu ikiwa na kutimiza majukumu yao kwenye upande wa malezi ya familia pamoja na ndoa zao, huku wakifanya kazi za kujiingizia kipato.

Alisema kuwa wanawake wana wajibu mkubwa wa kujishughulisha katika kuhakikisha wanakuwa walezi kwenye familia zao ikiwa na pamoja na kufanya miradi ya kujiingizia kipato.

Alisema pamoja na kazi kubwa ya kumtumikia Mungu, pia wanatakiwa kuhakikisha wanawajibika katika kuzifanya shughuli mbalimbali ambazo zitakazowainua kiuchumi badala ya kuwaachia wanaume kana ndiyo wanaostahili.

"Hapa ninazungumza na wanawake kutoka madhehebu mbalimbali ya dini, ni imani yangu maombi hayo ambayo tumeomba yataendelezwa na Mungu atatuponya na corona, ambayo imekuwa tishio duniani kote," alisema.



# CCM: Bila mbinu majimbo haya tungepoteza

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimekiri kuwa majimbo ya Mbeya Mjini na Mbarali, ndio yaliyokuwa magumu zaidi wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na madiwani uliofanyika, Oktoba mwaka jana.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, aliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha Halmashauri Kuu ya chama hicho kilichokuwa na lengo la kufanya uteuzi wa wagombea watakaoziba nafasi zilizoachwa na baadhi ya viongozi waliojiuzulu na waliofariki dunia.

Alisema majimbo hayo yalikuwa magumu kwa chama hicho hali iliyosababisha viongozi wa chama kufanya kazi kubwa kuhakikisha majimbo hayo yananyakuliwa na chama hicho.

Aliwapongeza wajumbe wa Halmashauri Kuu ya chama hicho kwa ushirikiano walioonyesha wakati wa uchaguzi huo hasa katika Jimbo la Mbeya Mjini ambalo kwa miaka 10 lilikuwa linaongozwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), chini ya Joseph Mbilinyi 'Sugu'.

"Kule Mbarali mwenzetu wa upande wa pili alitaka kutuzidi maana alikuwa vizuri sana kiuchumi na pengine tusingekuwa na akili nyingi za kichama tungezidiwa kule na hatuwezi kuficha kwa sababu tuliponea kwenye tundu la sindano," alisema Mwakasole.

Hata hivyo, alisema katika Jimbo la Mbarali kuna baadhi ya wanachama wa CCM waliungana na wapinzani kutaka kumwangusha mgombea wa chama hicho na kwamba ugumu mwingine ulisababishwa na mgombea wa CCM kuwa mgeni kwenye siasa.

Alisema chama hicho kina kazi kubwa ya kuhakikisha utekelezaji wa Ilani unafanyika kwa viwango ili kurahisisha kazi ya kukinadi tena chama hicho kwenye uchaguzi wa 2025.

Alisema kitendo cha kushinda majimbo yote ni mtihani mkubwa kwa chama hicho kwa maelezo kuwa wananchi wana imani kubwa na chama hicho hivyo lazima makada wa chama hicho wanatakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano katika utekelezaji wa ilani na ahadi za chama.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, Bashiru Madodi, alisema uteuzi wa wagombea wa nafasi za ndani ya chama hicho unahusisha wagombea wa jumuiya zote za chama ambazo hazina viongozi kutokana na sababu mbalimbali.

Alisema mchakato wa uteuzi wa wagombea wa nafasi zingine zote utafanywa na Halmashauri Kuu ya chama hicho ngazi ya mkoa isipokuwa nafasi ya Mwenyekiti wa chama Wilaya ya Kyela ambayo vikao vyenye maamuzi ya mwisho ni Halmashauri Kuu ya chama taifa.

Alisema katika Wilaya ya Kyela, Mwenyekiti wake alikuwa ni Ally Jumbe ambaye aligombea ubunge katika jimbo hilo na akashinda na kwamba nafasi yake inatakiwa kujazwa kutokana na chama hicho kuwa na utaratibu wa mtu mmoja kuwa na nafasi moja.

"Ipo pia nafasi ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa CCM (UWT), Wilaya ya Rungwe ambayo ipo wazi kutokana na aliyekuwa anaishikilia kufariki, lakini zipo nafasi kwenye ngazi za kata," alisema Madodi.

Kwa upande wake Katibu wa Umoja wa Vijana wa Chama hicho (UVCCM) Mkoa wa Mbeya, Twalib Belege, alisema uchaguzi wa viongozi hao unatarajiwa kufanyika kuanzia Machi 10 - 13, kulingana na ngazi ya uongozi.



Maofisa wa afya wakipulizia 'sanitizer' kwenye kipaza sauti kabla ya kuanza kutumiwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika (kushoto), ili kuepuka kuambukizana magonjwa ya mfumo wa hewa, wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Ukimwi, Kifua Kikuu na Dawa za Kulevya, jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Serikali yaridhia ujenzi mradi wa maji Mto Kiwira

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

SERIKALI imeridhia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-UWSSA) kuanza ujenzi wa mradi wa maji wa chanzo cha Mto Kiwira wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 70 ambao unatarajiwa kumaliza tatizo la maji katika mikoa ya Mbeya na Songwe.

Mradi huo unatarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2021/2022 na mamlaka hiyo imeagizwa kuanza maandalizi ya ununuzi ya vifaa ili kuhakikisha utekelezaji wake unaendana na muda.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Antony Sanga, alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara kwenye chanzo cha Mto Kiwira na kusema mradi huo utakamilika ndani ya miezi 24 kuanzia Julai, mwaka huu.

"Mradi huu ni lazima tuutekeleze na unahitaji fedha nyingi, sasa lazima muanze maandalizi mapema ili mwaka wa fedha unapoanza mwezi Julai na Agosti utekelezaji uanze na wananchi waanze kupata maji haraka," alisema Sanga.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha inamaliza matatizo ya maji kwa wananchi hasa wanawake kwa kuwasogezea huduma karibu na makazi yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mbeya-WSSA, Gilbert Kayange, alisema kwa sasa baadhi ya maeneo ya Jiji la Mbeya wananchi wanapata maji kwa mgawo kutokana na vyanzo vilivyopo kutokidhi mahitaji.

Alisema mradi huo ukikamilika utamaliza kabisa kero ya maji kwa wananchi wa jiji hilo na mengine yatapelekwa katika miji mingine ya Mkoa wa Mbeya na Songwe huku akisisitiza kuwa chanzo hicho kina maji mengi na bora.

Alisema mradi huo utakamilika haraka na wananchi kuanza kunufaika nao kutokana na hatua kusafirisha maji kwa njia ya mserereko ambayo ni nafuu zaidi kwenye uendeshaji.

"Huduma ya majisafi na usafi wa mazingira inaanzia kuwa na vyanzo vyenye maji ya kutosha, sasa mmejionea wenyewe chanzo hiki kina maji mengi sana ambayo yatatosheleza wananchi wa Jiji la Mbeya na hata miji mingine," alisema Kayange.

Aliahidi kuanza utekelezaji wa agizo la Katibu Mkuu la kuanza ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa mradi huo yakiwamo mabomba ili muda utakapofika ujenzi uanze mara moja.

Meneja Ufundi wa Mbeya-WSSA, Mhandisi Barnabas Konga, alisema chanzo hicho kina uwezo wa kutosheleza mahitaji ya wananchi wa Jiji la Mbeya na miji mingine ambayo ipo kwenye mradi huo kwa muda wa miaka 20 ijayo bila kuhitaji chanzo kingine.

Alizitaja halmashauri zingine zitakazonufaika na mradi huo kuwa ni ya Rungwe, Mbeya na Chunya kwa Mkoa wa Mbeya pamoja na Mbozi, Momba na Tunduma kwa Mkoa wa Songwe.

Alisema mradi huo utakuwa na uwezo wa kuzalisha maji yenye ujazo wa mita 365,000 kwa siku, lakini mahitaji ya Jiji la Mbeya ni mita za ujazo 79,000.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Wilaya ya Rungwe, Mnkondo Bendera, aliomba serikali kuhakikisha vijiji vyote vya wilaya hiyo ambavyo vitapitiwa na mradi huo kuwa sehemu ya wanufaika kwa maelezo kuwa na wao wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa huduma hiyo.

# Wakosa mawasiliano baada barabara kusombwa maji

**Na Nebart Msokwa, MBARALI**

WANANCHI wa kata tatu za Utengule Usangu, Luhanga na Igurusi, wilayani Mbarali, hawana mawasiliano ya barabara baada ya barabara kuu inayounganisha kata hizo kusombwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua.

Kukatika kwa barabara hiyo kumesababisha baadhi ya shughuli za kijamii na kiuchumi kusimama kutokana na vyombo vya usafiri hususan magari kushindwa kupita.

Hali hiyo ilisababisha gari lililokuwa likisafirisha mgonjwa kutoka Kata ya Utengule Usangu aliyekuwa amepewa rufani ya kwenda Hospitali ya Misheni Chimala, kukwama na kusababisha wananchi kujitokeza kuweka vifusi kwa kutumia jembe la mkono ili kuwezesha gari hilo kupita.

Wakizungumza wakati wa kuweka vifusi, baadhi ya wananchi waliiomba serikali kuwasaidia kuifanyia matengenezo barabara hiyo ili iwe inapitika katika kipindi cha mwaka mzima.

Haji Bakari, Mkazi wa Kijiji cha Iduya, wilayani Mbarali, alisema barabara hiyo ina umuhimu mkubwa kiuchumi kwa vile ndiyo wanayoitumia kusafirisha mazao kutoka mashambani na pia kwenda kwenye mnada mkubwa wa Luhanga unaofanyika mara mbili kwa wiki.

"Mbali na kuwepo kwa kituo cha afya, lakini katika Kata ya Luhanga kuna mnada ambao unafanyika mara mbili kwa wiki, watu wanaokwenda mnadani kufanya biashara wanashindwa kupita kutokana na ubovu wa barabara, lakini hata mazao yetu yanakwama kusafirishwa kutokana na barabara hii kuwa mbovu," alisema Bakari.

Alisema serikali pia inakosa fedha nyingi kutokana na kushindwa kukusanya vizuri ushuru kutoka kwa wafanyabiashara wanaofika kununua mazao katika maeneo hayo.

Kwa upande wake Mwina Mfumbilwa, mkazi wa Kata ya Utengule Usangu, alisema yeye na wanawake wenzake wanaogopa kushika mimba wakihofia usalama wao endapo watapata matatizo wakati wa kujifungua kwa vile hawataweza kupata usafiri wa kwenda hospitalini. "Tunaogopa kushika mimba kwa sababu ikiwa tutajifungua katika kipindi kama hiki ambacho barabara haipitiki tunahisi tunaweza kupata hasara kubwa ikiwamo kupoteza maisha," alisema Mwina.

Baadhi ya wawekezaji na vijana wanaotumia barabara hiyo kwa shughuli za kiuchumi nao walisema kuwa wanapata hasara kubwa kutokana na ubovu wa barabara hiyo.

Idd Chaula, mwekezaji wa mashine za kusindika mpunga katika Kata ya Luhanga, alisema anashindwa kukoboa mpunga na kusafirisha mchele kwenda Dar es Salaam kuuza kutokana na barabara hiyo kutopitika katika kipindi hiki cha mvua.

## Waandishi wapewa somo matumizi ya mikataba

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MRAJISI kutoka Tume ya Utangazaji Zanzibar, Shekha Haji Dau, amewataka waandishi wa habari kutumia maandiko ya mikataba mbalimbali ambayo nchi imeridhia wakati wa kuandika habari zao ili jamii ifahamu kwa kina masuala ambayo wanayazungumzia.

Aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya kukuza na kuwawezesha vijana wanawake na wanahabari katika vyombo vya habari kuhusu vitendo vya ukatili na udhalilishaji yaliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA).

Alisema Tanzania imeridhia mikataba mbali mbali ikiwamo ya kupinga ubaguzi ambayo ni muhimu kuitumia katika habari zao ili jamii kuelewa zaidi kile ambacho wanakiandika na kujua umuhimu wake.

Aliwataka waandishi wa habari kutumia kalamu zao kwa kuandika na kuzungumzia masuala ya jinsia kwa kuibua mambo mbalimbali ambayo yanahitaji kuibuliwa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Rose Rueben, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo kwa waandishi ili kuwajengea uwezo wa kuandika habari za kuwatetea wananchi.

Alisema mradi huo unelenga pia kuwafahamisha waandishi kufanya kazi zao bila kupata tatizo katika vyombo vya habari.

"Yapo matukio ya udhalilishaji yanayowakumba waandishi wa habari wanawake katika vyombo vya habari, lakini hushindwa kuyaripoti," alisema.

Mradi huo unalengo la kukuza na kuwawezesha wanawake wanahabari na vijana kwenye vyombo vya habari kutekeleza majukumu bila ya kuathiriwa husus an katika masuala ya udhalilishaji wa kingono.

# Uwekezaji kidigitali kupunguza mianya ya rushwa wawekezaji

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uwekezaji na Uchumi, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema kuanzishwa kwa mfumo maalum wa uwekezaji kwa njia ya kidigitali uchumi wa Zanzibar utakua kwa kasi, kutokana na wawekezaji wengi kujitokeza kwa wingi.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua mafunzo kwa ajili ya maofisa 20, kutoka Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar, ikiwa ni hatua ya kujipanga vyema kiutendaji yaliofanyika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Mazizini Zanzibar.

Alisema mfumo huo utapunguza kero kwa wawekezaji ya kuchukua muda mrefu wa kukamilisha taratibu zote, kuondoa mianya ya rushwa, kutaongeza idadi ya wawekezaji, pato la taifa na kuongeza wigo wa kibiashara.

Alisema malengo ya serikali ni kuongeza mapato kupitia nyanja mbalimbali ikiwamo ya uwekezaji na kwamba haitapendeza kuona kuna watendaji wanakwenda kinyume na malengo hayo.

Alisema katika kufanikisha hilo kazi kubwa imefanyika ya kuandaa na kubadilisha sera na sheria mbalimbali ili kuruhusu uwekezaji na kutoa fursa zinazohitajika kwa uhakika na haraka.

Pia alisema hiyo ni hatua kubwa katika maendeleo ya nchi yao na kushuhudia mageuzi makubwa ya teknolojia katika upatikanaji wa huduma.

"Kwa ujumla sote ni watumiaji wa teknolojia hizo kwa njia moja au nyingine hususan rika ya vijana ambao teknolojia wameikuta inaendelea kukua kwa kasi mno," alisema.

Aliyataja miongoni mwa mabadiliko na mambo ya mfano yaliyo hai ni pamoja na upatikanaji wa huduma za kibenki, huduma za umeme na uhaulishaji wa fedha, huduma ambazo zimekuwa zikifanyika kwa kutumia simu ya mkononi kwa wepesi na urahisi na bila ya usumbufu wowote.

Naye Katibu Mkuu, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mussa Haji Ali, alisema kuanzishwa kwa mfumo huo kuna lengo la kuongezeka kwa ufanisi na utendaji kazi mzuri kwa wafanyakazi, pamoja na kuongeza imani kwa wawekezaji ya kufika Zanzibar kwa lengo la kuwekeza.

Alisema katika kuhakikisha mfumo huo unaleta tija, serikali imefanya majaribio ya matumizi ya mfumo wa kidigitali kwa wafanyabiashara wa ndani wenye kupata faida na kuonekana mfumo huo una tija kubwa.

Kwa upande wa mjumbe wa kamati maalum ya waandaaji mfumo huo, Dk. Yahya Hamad Shehe, alisema matarajio ya awali kwamba mradi huo uanze kazi Desemba mwaka jana, lakini kutokana na mlipuko wa maradhi ya corona ilishindakana, kutokana na baadhi ya vifaa na wataalamu kushindwa kufika Zanzibar.

Mafunzo hayo ya wiki mbili yamewashirikisha watendaji wa serikali wanaotoa huduma za uwekezaji ambayo matarajio ya serikali kwa sasa ni mwekezaji kuwasilisha ombi la huduma anayoihitaji na kupokea majibu ya ombi hilo kwa njia ya mtandano, hatua ambayo itaondoa kero na usumbufu kwa wawekezaji bila kuathiri matakwa ya msingi ya kisheria katika upatikanaji wa huduma hizo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Dk. Saada Mkuya, akisaini kitabu cha wageni wakati alipofanya ziara katika Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mkuya aelekeza mapambano dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, amewataka watendaji na wafanyakazi wa Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya Zanzibar kuongeza juhudi na mapambano dhidi ya wanaoingiza, kuuza na kusambaza kwa maslahi ya Zanzibar.

Aliyasema hayo jana wakati alipokutana na uongozi na wafanyakazi wa Tume hiyo na kuwataka kuwa waadilifu na waaminifu kwa vile vita vya matumizi ya dawa za kulevya ni kero na mtandao wake ni mkubwa.

Katika kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo, Dk. Saada, aliwataka kuzidisha ushirikiano na taasisi mbalimbali wanazofanya kazi kwa ukaribu ikiwamo uwanja wa ndege, bandarini na kusambaratisha mitandao ya wahalifu.

Alieleza hivi sasa fursa nyingi za maendeleo zinapatikana zikiwamo utalii, ujenzi wa miundombinu ambazo zimekuwa zikiibua fursa mbalimbali za kiuchumi.

Aliwataka watendaji hao kufanya tathmini ya wanachokitoa hatua ambayo itasaidia kufahamu upungufu yaliyopo kwa upande wao.

Hata hivyo, alisema atahakikisha anashirikiana na watendaji na anasimamia vyema sheria na sera ikiwamo kuzipitia upya na kufanya marekebisho pale panapohitajika kufanya hivyo ili kuwabana wahalifu na kuifanya jamii na serikali iwe huru.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Tume hiyo, Kheriyangu Mgeni Khamis, alisema pamoja na mambo mengine Tume imefanikiwa kuteketeza dawa za kulevya kitaalamu, kuanzishwa kwa nyumba za kurekebisha tabia, kufanya marekebisho ya Sheria 2019 na kubadilisha vifungu vya adhabu, kuimarisha ushirikiano wa kitaifa na kimataifa.

Wakati huo huo, waziri alitembelea Tume ya Ukimwi Zanzibar na kuwaomba kuharakisha kutoa mwongozo na kufanyiwa kazi ikizingatiwa watendaji wakuu wengi ni wapya ili wapate fursa ya kuupitia.

Aliwataka watendaji wa Tume hiyo wasiridhike na kiwango cha maambukizi cha sasa cha asilimia 0.4 kwa vile mwingiliano ni mkubwa hasa kwa wakati huu ambao Zanzibar inapata wageni wengi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Ukimwi, Dk. Ahmed Mohammed Khatib, alisema moja kati ya mafanikio ya Tume ni jamii kuelimika, kupungua kwa unyanyapaa na kuvuka kiwango cha asilimia moja ikilinganishwa na mataifa mengine ambayo kiwango huwa juu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ANAHITAJIKA PHARMASIA

**KAMPUNI YA DAWA ILIYOPO DA ES SALAAM INAHITAJI PHARMASIA/ PHARMASIA MSAIDIZI.**

**KWA MAWASILIANO ZAIDI: NAMBARI: 0713 786 300**

## MAENEO YA KUJENGA SHELL YANAUZWA

**Yombo Buza, Mwanagati, Mbande, Tandika, Kigamboni, Kibaha na Bagamoyo.**

**Wasiliana na TANLANDS. SIMU: 0686 302219 0686 373022**

## MASHAMBA YANAUZWA

**Kibaha, Msata, Kisarawe, Soga, Kigamboni, Mkuranga na Bungu.**

**Wasiliana na NJANI PROPERTY COMPANY (NPC). SIMU: 0628 336736 / 0657 990015**

## VIWANJA VINAUZWA

**Kibaha, Kisarawe, Chanika, Kigamboni, Malela, Kisemvule, na Bungu.**

**Wasiliana na NJANI PROPERTY COMPANY (NPC) SIMU: 0628 336736 / 0657 990015**

## NYUMBA ZINAUZWA

**Yombo Buza, Kibaha, Mbezi, Kitunda, Chanika, Tabata na Kinyerezi.**

**Wasiliana na Tanlands Real Estate Agency. Simu: 0686 302219 / 0692 006546**

---

**THE COMPANIES ACT NO. 12 OF 2012**
**AFRICA OCCUPATIONAL HEALTH AND SAFETY SPECIALISTS LIMITED**

**TAARIFA KWA UMMA**

Tunapenda kutoa tangazo kwa umma kuwa Kampuni ya **AFRICA OCCUPATIONAL HEALTH AND SAFETY SPECIALISTS LIMITED** yenye usajili **Na. 92003** iliyo na Ofisi zake maeneo ya Jiji la Dar es salaam, inafungwa kwa hiyari ya wanahisa wenyewe. Hivyo tunaomba kama kuna Taasisi au mtu yeyote ana madai awasiliane na sisi kupitia anwani ifuatayo, ndani ya siku **14** tangu tarehe ya kutolewa tangazo hili.

**Mkurugenzi**
**AFRICA OCCUPATIONAL HEALTH AND SAFETY SPECIALISTS LIMITED**
**P.O. Box 76401**
**Dar es salaam.**

---

**THE COMPANIES ACT NO. 12 OF 2012**
**HERRYSON COMPANY LTD**

**TAARIFA KWA UMMA**

Tunapenda kutoa tangazo kwa umma kuwa Kampuni ya **HERRYSON COMPANY LTD** yenye usajili Na. 104758 iliyo na Ofisi zake maeneo ya Jiji la Dar es salaam, inafungwa kwa hiyari ya wanahisa wenyewe. Hivyo tunaomba kama kuna Taasisi au mtu yeyote ana madai awasiliane na sisi kupitia anwani ifuatayo, ndani ya siku 14 tangu tarehe ya kutolewa tangazo hili.

**Mkurugenzi**
**HERRYSON COMPANY LTD**
**P.O. Box 76401**
**Dar es salaam.**

---

**THE COMPANIES ACT NO. 12 OF 2012**
**BLUELINE TRANSPORT LIMITED**

**TAARIFA KWA UMMA**

Tunapenda kutoa tangazo kwa umma kuwa Kampuni ya **BLUELINE TRANSPORT LIMITED** yenye usajili **Na. 66079** iliyo na Ofisi zake maeneo ya Jiji la Dar es salaam, inafungwa kwa hiyari ya wanahisa wenyewe. Hivyo tunaomba kama kuna Taasisi au mtu yeyote ana madai awasiliane na sisi kupitia anwani ifuatayo, ndani ya **siku 14** tangu tarehe ya kutolewa tangazo hili.
Mkurugenzi

**Mkurugenzi**
**BLUELINE TRANSPORT LIMITED**
**P.O. Box 76401**
**Dar es salaam.**

---

**THE COMPANIES ACT NO. 12 OF 2012**
**H & M MICROFINANCE CO. LTD**

**TAARIFA KWA UMMA**

Tunapenda kutoa tangazo kwa umma kuwa Kampuni ya **H & M MICROFINANCE CO. LTD** yenye usajili **Na. 103186** iliyo na Ofisi zake maeneo ya Jiji la Dar es salaam, inafungwa kwa hiyari ya wanahisa wenyewe. Hivyo tunaomba kama kuna Taasisi au mtu yeyote ana madai awasiliane na sisi kupitia anwani ifuatayo, ndani ya **siku 14** tangu tarehe ya kutolewa tangazo hili.

**Mkurugenzi**
**H & M MICROFINANCE CO. LTD**
**P.O. Box 76401**
**Dar es salaam.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALEX BUGAMI MENYEYE**

Wa igomelo Mjini Kahama, anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya HIACE rangi nyeupe, yenye namba za usajili **T. 374 DVJ**, yenye Chassis **No. RZH1254009911,** Engine No. **2RZ2933253**. Yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya jeshi la polisi. **KAH/RB/1010/2021.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MÀHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NO 24/2021**
**MDAI ALOYCE MWANKUPILI**
**DHIDI YA**
**MDAIWA GODLOVE KIHONGUSI**
**KWA GODLOVE KIHONGUSI WA FIRE MOROGORO**
**Ombi la Mdai ALOYCE MWANKUPILI**
**Madai ya pesa 8,512,000Tshs**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauril tajwa hapo juu bila kukosa.
Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 9 Mwezi 3 Mwaka 2021 saa 8:30 Asubuhi.

Angalia Kama*hukuhudhuria/hamtohudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha Kama Umepokea/ Mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Màhakama hii leo tarehe 23 Mwezi 02 Mwaka 2021

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO.

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GEOFREY R. MWASAKAFYUKA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.822 DMR.** Yeyotete atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/133858/2021.**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.60/2021**

Ombi la **EUNICE JAMES SHANGALI** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **MARTIN JAMES SHANGALI**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **12/04/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 03/03/2021**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHUBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA 94 YA MWAKA 2020**
**MOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**TULAMWONA SIMON MKINI-MAREHEMU**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**PHILBERT BAPTISTER MICHAEL**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia masharti haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimaiiz wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 8 mwezi **MARCH mwaka 2021**
**Imewasilishwa dar es salam leo 8 mwezi wa 2 mwaka 2021**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya**
**DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na 14/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU RUKIA MOHAMED ABDALLAH WA AREA 'A'DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA NAJMA ABDALLAH MWINYIMKUU.**

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo **tarehe 30 mwezi 03 mwaka 2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 09 mwezi 03 mwaka 2021.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya**
**DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na 13/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU IBRAHIM JUMA KIVINA WA AREA 'A'DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SOPHIA IBRAHIM KIVINA**

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 25 mwezi March mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 09 mwezi 3 mwaka 2021.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya**
**DODOMA MJINI**
**Kituo cha DODOMA Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi 52/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HAWA RAJABU WA DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA FAMY HINDI ATHUMANI**

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 10/03/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo Tarehe 4 mwezi 3 mwaka 2021.**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHUBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA 95 YA MWAKA 2020**
**MOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**BAPTISTER MICHAEL LUDALO -MAREHEMU**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**JOEL BAPTISTER MICHAEL**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia masharti haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimaiiz wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 8 mwezi **MARCH mwaka 2021**
**Imewasilishwa dar es salam leo 8 mwezi wa 2 mwaka 2021**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO**
**MAOMBI NA. 8 YA 2021**
**IDDI AYUBU**
**ASMA MGUMBA ............WALETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**MAHAMUDU MATAULA.........MJIBU MAOMBI**
**WITO/ KUITWA SHAURINI KWA MAHAMUDU MATAULA**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro **tarehe 18/3/2021** wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukuosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautohudhuria maombi yatatajwa na kukilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetokea kwa mkono wangu leo tarehe 9 Mwezi March 2021

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**MOROGORO**

---

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe

## OFISI ZA MATANGAZO
## MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

## HABARI KIMATAIFA

# Vifo mlipuko kambi ya jeshi Guinea vyaongezeka

**Bata,** EQUATORIAL GUINEA

VIFO vimeongezeka baada ya kutokea mfululizo wa milipuko katika kambi za jeshi Equatorial Guinea na kufikia zaidi ya watu 98.

Kwa mujibu wa taarifa ya wizara ya afya kwa watu waliojitolea wanaendelea kutafuta maiti katika vifusi Shirika la Habari la Reuters, liliripoti.

Takriban watu 615 walijeruhiwa katika mlipuko wa Jumapili, ambao ulianza na moto katika kambi ya jeshi ya Nkoantoma, katika mji wa Bandari wa Bata, kwa mujibu wizara ya ulinzi.

**Kati ya waliojeruhiwa 299 walilazwa hospotalini kwa mujibu wa ujumbe wa Twitter wa wizara ya afya.**

Akimnukuu Makamu wa Rais, wizara ya afya ilisema idadi ya vifo imefikia zaidi ya watu 98, ikiwa ni zaidi ya mara tatu ya idadi iliyokadiriwa awali ya vifo 31.

Kati ya waliojeruhiwa 299 walilazwa hospotalini kwa mujibu wa ujumbe wa Twitter wa wizara ya afya.

Rais Teodoro Obiang Nguema, ambaye ni baba wa makamu wa rais, alizungumzia ajali hiyo kuwa ni uzembe unaotokana na kushughulikia vibaya milipuko.

Aliongeza kwamba mlipuko huo umeharibu karibu nyumba zote na majengo Bata, mji ambao una idadi ya watu 250,000.

Wizara ya Afya ya Equatorial Guinea, ilitoa ujumbe wa Twitter ambao ulieleza kwamba imeandaliwa timu ya wataalamu wa magonjwa ya akili inayoundwa na wanasaikolojia, madaktari wa akili na wauguzi ili kushughulikia waathirika wa mlipuko huo.

Picha zilizochapishwa na vyombo vya habari vya nchini humo, zilionyesha maiti zikiwa zimefungwa katika mashuka na kuwekwa pembezoni mwa barabara, huku watoto wakiwa wametolewa katika mabaki ya majengo. **VOA**



Nyumba zilizoharibiwa baada ya mlipuko ulitokea juzi na kusababisha takribani vifo vya watu 100 katika kambi ya jeshi mjini Bata, Equatorial Guinea. **PICHA: BBC**

# Prince Harry akosoa ubaguzi vyombo habari

**Washington,** MAREKANI

MWANAMFALME Harry, amesema ubaguzi wa vyombo vya habari uliojipenyeza hadi jamii zingine, ndio sababu kubwa yeye na mkewe kuondoka nchini Uingereza.

Mwanamfalme Harry (pichani) alimwambia Oprah Winfrey kwamba vyombo vya habari Uingereza vina ubaguzi na hutengeneza mazingira yasioweza kuvumilika ili kudhibiti hofu.

Alisema alifikiria kwamba Mwanamfalme Charles wa Wales ambaye ni baba yake, alilazimika kuhakikisha ana amani navyo.

Hata hivyo wahariri walisema kuwa vyombo vya habari havina ubaguzi vinahakikisha kuwa familia ya kitajiri na inawajibika.

Katika mahojiano yao na Oprah, Harry na mkewe Meghan, walisema kwamba baada ya kusitishwa kwa ufadhili wao na Familia ya Kifalme, tajiri wa Marekani Tyler Perry aliwapa hifadhi ya makazi na ulinzi, eneo la California mwaka jana.

Tyler Perry alijitolea kuishi na wanandoa hao bure katika moja ya majumba yake ya kifahari na kutuma ulinzi wake walipokuwa wanahama kutoka Canada hadi Los Angeles.

Walisema katika mahojiano yao maalum na shirika la habari la CBS nchini Marekani, Jumapili.



Wanandoa hao walisema waliamua kuondoka baada ya eneo la nyumba waliokuwa wanaishi kisiwa cha Vancouver, Magharibi mwa Canada kufahamika na watu wengi.

"Hatukuwa na mpango wowote," Meghan alisema katika mahojiano.

"Tulihitaji nyumba na Tyler Perry alijitolea kutusaidia na maofisa wake wa ulinzi pia na hilo likatupatia fursa ya kupumua na kufikiria hatua tutakayochukua."

"Ghafla ikanijia akilini kwamba: Nikafikiria kwa haraka, mipaka inaweza kufungwa, ulinzi wetu utaondolewa na hakuna anayejua hatua ya kufungiwa itaendelea kwa muda gani, dunia inajua tuko wapi, sio salama na bila shaka tutahitajika kuondoka hapa."

Harry na Meghan walisema kwamba baadaye, waliamua kwenda kuishi California na kununua nyumba Montecito.

Perry (51) ni mtengenezaji filamu mashuhuri, mchekeshaji, mwigizaji, mzalishaji wa vipindi na mtunzi.

Perry anafahamika kwenye filamu za Madea alizoandika, akazisimamia, mwelekezi na aliyeshiriki kama mhusika mkuu, mwanamke mzee anayetumia viungo bandia. **BBC**

## Simba waua ofisa wanyamapori

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

OFISA wanyamapori, amefariki baada ya kushambuliwa na simba wawili katika hifadhi ya wanyama nchini Afrika Kusini, mamlaka zimesema siku ya Jumatatu.

Malibongwe Mfila, 27, ambaye alifanya kazi ya kufuatilia mienendo ya wanyama katika mbuga ya kitaifa ya wanyama ya Marakel, alikuwa akiwatafuta wanyama katika mbuga hiyo siku ya Jumamosi aliposhambuliwa na simba hao.

Polisi walisema alikuwa akiendesha gari kuwatafuta wanyama kama vile simba na tembo ili kutoa ushauri kwa wanaowaelekeza watalii mbugani.

Aliamua kuacha gari na kuendelea kuwatafuta wanyama kwa miguu, mara ghafla akashambuliwa na simba wawili hadi kufariki.

Simba hao pia waliuawa kwa kupigwa risasi.

Mwaka jana, mtunzaji mashuhuri wa Afrika Kusini Mathewson Magharibu, alifariki baada ya kushambuliwa na simba alipokuwa akiwapeleka matembezi wageni katika Hifadhi ya Wanyama ya Limpopo. **BBC**

## HRW yaitaka Burundi kuwaachia wahamiaji

**Bangui,** CAR

SHIRIKA la Kutetea Haki za Binadamu la Human Rights Watch, limezitaka mamlaka za Burundi kutupilia mbali lilichokiita mashtaka yasiyo na msingi na ziwaachilie huru wakimbizi waliorudishwa nchini humo kwa lazima.

Februari 26, mwaka huu, mahakama ya Muha mjini Bujumbura ilifanya uamuzi wa kutowaachilia wahamiaji hao.

Upande wa mashtaka haukuwasilisha ushahidi wa kuthibitisha haja ya kuendelea kushikiliwa kwa wahamiaji hao. Isitoshe kumekuwa na ukiukwaji wa mara kwa mara wa haki kuhusu mchakato wa kisheria dhidi yao.

Lewis Mudge ambaye ni mkurugenzi mkuu wa Human Rights Watch, tawi la Afrika ya Kati (CAR), alisema taifa la Burundi linaongeza chumvi kwenye kidonda kwa kushtaki kundi la wahamiaji.

Aliongeza kwamba mashtaka hayo yasiyo na msingi yanaonesha jinsi kurudishwa kwa wahamiaji hao kumeingiliwa kisiasa na utawala nchini Burundi unadhibiti mahakama.

Wahamiaji wanaoshtakiwa walidai waliteswa. Wanne kati yao kwa wako katika Gereza la Bubanza na wengine wanne wako Gereza la Muramvya. **DW**

# YOUNG KURUDI WATFORD




**MILAN,** Italia

WINGA wa zamani wa timu ya Taifa ya England, Ashley Young ametajwa kwamba anatarajiwa kurudi katika klabu yake ya kwanza nchini England, Watford.

Young mwenye umri wa miaka 35, kwa sasa ana matumaini ya kubeba ubingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie, A akiwa na Inter Milan, kabla ya kurejea kwenye Ligi Kuu England.

Young ambaye alipita kucheza kwenye timu za Aston Villa, Manchester United na sasa Inter awali katika maisha yake ya soka la kulipwa alianza kuitumikia Watford na anaamini hiki ni kipindi cha kurejea nyumbani ikiwa ni nyakati zake za mwisho kabla ya kutundika daluga.

"Tupo kwenye nafasi nzuri ya kubeba taji la Ligi Kuu Italia, na baada ya hapo nina mawazo tofauti," alisema Young akinukuliwa na Sky Sport Italia.

# Klopp atoa neno kufukuzwa Liverpool

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Kloop amesisitiza kuwa ikiwa atafutwa kazi ndani ya timu hiyo kwa sasa kutokana na mwendo mbovu wa timu hiyo, haoni mtu wa kubeba mikoba yake ambaye anaweza kufanya vizuri zaidi yake.

Mwendo ambao anakwenda nao kwa sasa ndani ya Liverpool ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England, unafananishwa na ule wa msimu wa 2014/15 wakati alipokuwa akikinoa kikosi cha Borussia Dortmund ambacho kinashiriki Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Klopp kwa sasa kikosi chake asilimia kubwa nyota wake wa kikosi cha kwanza wanatibu majeraha ya muda mrefu ambapo huduma ya nyota wake, Virgil van Dijk, Joe Gomes na Joe Matip ambao bado hawajarejea ndani ya uwanja anakosa huduma yao.

Kocha huyo amesema wapo watu ambao wanafikiria ameishiwa mbinu na hawezi kufanya vizuri, jambo ambalo anaamini yeye ni kwamba hakuna anayeweza kubadili kila kitu hata akiletwa kocha mpya hawezi kufikia ubora wake.

"Nadhani kwamba kuna mtu anafikiri kwamba anaweza kuja kocha mpya hapa, sawa hilo sikatai kwa sababu mimi sina maamuzi. Lakini ipo wazi kabisa kwa kuwa wao wana maamuzi," alisema akinukuliwa na BBC Sport.

"Lakini ukweli ni kwamba, hakuna kocha ambaye anaweza kufanya vizuri, nadhani hakuna ambaye anaweza akafanya vizuri kwa namna ambavyo wanafikiri kwa sasa, bado ni lazima kuwa na muda wa kufikiria na kuamua hivyo ni suala la kusubiri.






# Man United yamwinda Varane

**MADRID,** Hispania

MANCHESTER United ipo kwenye mipango ya kutaka kumsajili mlinzi wa Real Madrid, Raphael Varane, kwa mujibu wa BBC Sport.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Man United wanaona kwamba, Varane anaweza kuwa msaada mkubwa wa kumsaidia nahodha na mlinzi wao wa kati, Harry Maguire.

Kwa siku za hivi karibuni, Maguire amekuwa akishutumiwa kwa kiwango kibovu na makosa mengi kwenye safu ya ulinzi ya timu hiyo, hali inayopelekea kufungwa mabao ya kizembe.

Na sasa United wamerusha karata yao hiyo wakiamini kwamba, David Alaba atakwenda kule Madrid kutoka Bayern Munich na hivyo wao watakuwa na nafasi kubwa ya kumsajili Varane.

Man United imekuwa ikisaka mlinzi wa kati huku pia ikihusishwa na Sergio Ramos ambaye mkataba wake unafikia mwisho, kipindi cha majira ya joto.

Hata hivyo, kwenye sakata la kumwania Ramos linaonekana kuwa gumu kwao, kwani Madrid wenyewe wameonyesha nia ya kutaka kuendelea naye, huku pia miamba ya soka ya Ufaransa, PSG wakitajwa kumuwania.

## HABARI MICHEZO

# Pochettino: Nautaka ubingwa wa UEFA

**PARIS,** Ufaransa

MAURICIO Pochettino ameahidi kwamba Paris Saint-Germain "itapambana hadi kufa" kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

PSG itatafuta nafasi yao katika robo fainali ya mashindano hayo wakati watakapowakaribisha washindi mara tano, Barcelona katika mchezo wa pili wa raundi ya 16, leo Jumatano.

Mabingwa wa Ufaransa walifika kwenye fainali msimu uliopita, lakini walipata kipigo kutoka kwa Bayern Munich msimu uliopita.

Lakini sasa, Pochettino ameazimia kuisaidia timu hiyo kupiga hatua zaidi kwenye mashindano hayo msimu huu kwa kulibeba taji hilo.

PSG iliifunga Leipzig bao 1-0 nyumbani kabla ya kupata ushindi mnono wa 3-1 dhidi ya 'Mashetani Wekundu' katika dimba la Old Trafford na kuichapa Basaksehir 5-1, na kukutana na Barcelona.

Kikosi cha Pochettino kisha kilipunguza kazi ngumu kwa kuigaragaza Bacelona 4-1 katika dimba la Camp Nou kwenye mchezo wa kwanza wa 16-bora, na watatarajiwa kumaliza kazi huko Parc des Princes leo, Jumatano.

Katika mahojiano na LFP, Pochettino amesema ana matarajio makubwa na kikosi hicho msimu huu.

"Ni wazi, ni matarajio ya klabu kushinda. Kuna timu nyingi ambazo zinataka kushinda, si rahisi. Tunafahamu jukumu letu na tutapambana hadi kufa ili kuifanikisha," alisema.

"Matumaini yangu ni kwamba, msimu huu, PSG italibeba Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza, na naona kabisa kila kitu kinawezekana."





# LACAZETTE AZIAMSHA BARCELONA, JUVENTUS

**LONDON,** England

IMERIPOTIWA kwamba nyota wa Klabu ya Arsenal, Alexandre Lacazette anawaniwa na timu nyingi zikiwamo na Barcelona, Juventus na Atletico Madrid.

Mkataba wa Lacazette ndani ya kikosi cha Arsenal kinachonolewa na Mikel Arteta, unafikia ukiongoni mwishoni mwa msimu huu wa 2020/21.

Nyota huyo amekuwa hana uhakika wa namba kwenye kikosi cha kwanza kwa kuwa wakati mwingine amekuwa akianza na mwingine akianzia benchi.

Mshambuliaji huyo amefunga jumla ya mabao nane ndani ya Ligi Kuu England msimu huu kwa kikosi hicho.

Habari zinaeleza kuwa nyota huyo yupo tayari kuondoka katika Ligi Kuu England ili kupata changamoto nyingine nje ya dimba la Emirates.

Hivyo, upo uwezekano akaibukia ndani ya Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa wababe Juventus ikiwa atakubali kusaini huko, ama ndani ya LaLiga kwa Barcelona ama Atletico Madrid ambazo zote zimeonyesha nia ya kuipata saini yake.

Kwa mujibu wa Calciomercato.com umeeleza kuwa Lacazette yupo tayari kuondoka ndani ya Arsenal mkataba wake utakapoisha.

# *Costa apewa ofa Benfica*

**LISBON,** Ureno

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Atletico Madrid na Chelsea, Diego Costa, amepewa ofa ya mkataba wa euro milioni tatu kwa mwaka na Benfica, vyombo vya habari vimethibitisha.

Costa kwa sasa amekuwa akitafuta klabu mpya, baada ya kuomba kuvunja mkataba wake na Ateltico Madrid Desemba mwaka jana.

Benfica sasa wanatafuta kuimarisha safu yao ya ushambuliaji kwa kumwongeza raia huyo wa Hispania kabla ya msimu wa 2021-22, wakiwa tayari wamewasiliana na mshambuliaji huyo kuweka masharti yao.

Vyanzo vya habari vinaripoti kuwa Benfica inataka kumfunga Costa kwa mkataba wa miaka miwili, ambayo inamaanisha atapata jumla ya mshahara wa euro millioni sita, ikiwa atahamia pale kwenye dimba la Da Luz.

Mshambuliaji huyo wa kati wa zamani wa Chelsea alikuwa akitajwa kurudi Ligi Kuu katika dirisha la uhamisho la Januari, huku klabu kama Manchester City, Tottenham na West Ham zikionyesha kuvutiwa naye.

Lakini, makubaliano ya mwisho hayakutokea na klabu nyingi ambazo zimekuwa zikihusishwa na huduma yake.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# TUCHEL AANIKA SABABU PULISIC KUSUGUA BENCHI

●●● Si suala la kumwamini au ubora wake, ni kwamba anatakiwa kuwa mpole na mtulivu tu...

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amesema Christian Pulisic amekuwa hana "bahati" kwa kukosa muda wa kucheza, lakini anahitaji kuwa mpole.

**Pulisic alikuwa nguzo muhimu ya 'Blues' hao msimu uliopita, lakini amekuwa na mechi chache za kucheza msimu huu chini ya kocha Tuchel, akitokea benchi kwenye mechi nne zilizopita.**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani, aliingia dakika ya 90 kuchukua nafasi ya Timo Werner wakati Chelsea ikiichapa Everton mabao 2-0 juzi, Jumatatu.

Tuchel, ambaye alifanya kazi na Pulisic wakati akiwa Borussia Dortmund, alifafanua kwamba hakuna kitu chochote kati yao, lakini ni suala la ushindani tu wa namba.

"Ndio, siwezi kusema chochote, lakini kuna vitu vizuri kuhusu yeye," alisema Tuchel.

"Pengine tatizo kubwa ni kwamba, namjua yeye tangu akiwa Dortmund.

"Ni jukumu langu na kwa kiasi fulani si sawa, lakini najua umuhimu wake akiwa uwanjani angalau kwa dakika 20 au 30. Alikuwa na bahati mbaya kwa michezo michache iliyopita.

"Si suala la kumwamini au ubora wake, ni kwamba anatakiwa kuwa mpole na mtulivu tu.

"Nina mtu mwingine ambaye naweza kumtaja ni Emerson ambaye naye anakumbwa na maamuzi yangu mabaya. "Hachezi lakini ni mtu wa aina yake kwenye mazoezi na huwa ana morali kubwa zaidi na timu na hajawahi kuniangusha.

"Yalikuwa maamuzi magumu kumweka nje ya kikosi cha leo (juzi) na nafasi yake akacheza Tammy (Abraham).

"Ni kama vile una kundi la wachezaji wazuri, lakini unapata wakati mgumu wa kuchagua wachezaji."

## ZISIKUPITE

### CITY YAJITOA KWA MBAPPE

MANCHESTER City haitafuatilia mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, 22, mwisho mwa msimu huu kwa sababu ya mahitaji ya mshahara wa mchezaji huyo.

### HAALAND, LUKAKU WAWINDWA

NYOTA wa klabu ya Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20 na mshambuliaji wa Inter Milan na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye miaka 27, wanawaniwa na Manchester City. ***(The Athletic)***

### JUVE, LIVER KWA HAALAND

STRAIKA wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, 20, ataamua timu atakayoichezea Ulaya mwishoni mwa msimu huu, huku Manchester United, Chelsea, Liverpool, Bayern Munich, Real Madrid na Juventus zote zikimnyatia mchezaji huyo. ***(ESPN)***

### MADRID KUMUUZA BALE JUMLA

KLABU ya Real Madrid inatumaini kwamba, kuimarika kwa kiwango cha mchezo wake, Gareth Bale, 31, katika klabu ya Tottenham Hotspur, kutarahisisha kumuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales kwa mkataba wa kudumu mwisho wa msimu huu. ***(Mail)***

### KLOPP AUNGWA MKONO

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, anaungwa mkono na mmiliki wa klabu hiyo, kundi la kampuni za Fenway, licha ya kiwango cha mchezo wa timu hiyo kushuka. ***(Times)***

### RAPHINA AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imemfanya mshambuliaji wa Leeds na Brazil, Raphinha, 24, kama mchezaji wanayemlenga mwishoni mwa msimu huu. ***(Todofichajes via Express)***

### LACAZETTE ASHAURIWA BARCA

WAKALA wa mshambuliaji wa Arsenal, Alexandre Lacazette, 29, amemtaka kujiunga na Atletico Madrid, Barcelona au Juventus. ***(Calciomercato)***

### CAVANI KUONDOKA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Edinson Cavani, 34, ameamua kwamba ataondoka Manchester United mwisho mwa msimu na kujiunga na Boca Juniors. ***(Ole)***

### AMAVI SASA KUTUA ARSENAL

ARSENAL itamsajili aliyekuwa beki wa Aston Villa, Jordan Amavi, 26, kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu huu, wakati mkataba wake utakapokamilika katika klabu ya Marseille. ***(Star)***

### MILENKOVIC AGOMBEWA EPL

MANCHESTER United, Tottenham na Liverpool zina nia ya kumsajili mlinzi wa Fiorentina mwenye umri wa miaka 23, Nikola Milenkovic. ***(Calciomercato)***

# MOROCCO NA MBINU MPYA KWA WAMOROCCO CAF LEO

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

WAKATI wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF), Namungo FC, leo saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki wakitarajia kushuka dimbani nchini Morocco kucheza na wenyeji wao, Raja Casablanca kwenye mechi ya kwanza ya Kundi C hatua ya makundi, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hemed Morocco, ameeleza mbinu watakazozitumia kuwavaa wakongwe hao.

Namungo ambayo ni mara ya kwanza inashiriki michuano hiyo, itakuwa inacheza mechi ngumu kutokana na historia ya timu za Afrika Kaskazini maarufu kama 'Waarabu', lakini historia ya timu hiyo ambayo ni moja kati ya timu ngumu, kongwe na zenye uwezo wa hali ya juu kisoka barani Afrika.

**Lakini Kocha Morocco, amesema kuwa amewaandaa vijana wake kimchezo, kimbinu na kisaikolojia kwani wanacheza na moja kati ya timu vigogo barani Afrika.**

"Tutaingia na tahadhari kwa kuwa tunafahamu tunakutana na timu ngumu, tunaomba Watanzania wazidi kutuombea dua. Wachezaji wangu wote wapo vizuri kuelekea katika mchezo huo na kila mmoja morali yake ipo juu," alisema.

Alisema alinasa baadhi ya mikanda ya video ya timu hiyo ya hivi karibuni na anaamini itamsaidia kimbinu kwa ajili ya kukabiliana na timu hiyo.

"Nimeyafanyia kazi mapungufu na ubora wa wapinzani wetu ili kupata matokeo chanya, lakini hata sisi tulikuwa na mapungufu yetu ambayo nayo tumejaribu kuyarekebisha, nadhani mambo yataenda vizuri," alisema.

Morocco alisema wanajua ubora wa wapinzani wao na hasa wakicheza nyumbani, hivyo amewatahadharisha vijana wake kuwa makini.

Mbali na Namungo na Raja Casablanca kwenye kundi hilo, pia kuna timu za Nkana FC ya Zambia na Pyramids ya Misri.

Timu hizo nayo zitakipiga nchini Misri muda huo huo ambao Namungo itakuwa inacheza dhidi ya Wamorocco hao.

Namungo ilifanikiwa kuingia hatua ya makundi kwa kuing'oa Clube Desportivo Primeiro de Agosto ya Angola kwa jumla ya mabao 7-5, huku Raja Casablanca ikiiondosha mashindanoni, US Monastir ya Tunisia kwa mikwaju ya penalti 6-5, baada ya kila moja kushinda nyumbani bao 1-0.




Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (wa pili kushoto) akikabidhi mbuzi anayekadiriwa kuwa na kilo 100 kwa mchezaji wa timu ya Mabody FC, Faraji Hassani, baada ya timu hiyo kutwaa ubingwa wa Kombe la Mbuzi kwa kuifunga Nyegezi FC kwa bao 1-0 katika mchezo wa fainali uliopigwa Uwanja wa Kumba juzi. Kushoto ni Katibu wa CCM Wilaya ya Pangani, Mohamed Moyo na kulia ni Mwenyekiti wa Chama cha Soka wilayani Pangani, Brahimu Selemani. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Polisi yatoa msimamo, KMKM yavutwa shati

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kukubali sare ya bao 1-1 dhidi ya Black Sailor katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyopigwa Uwanja wa Mau A juzi, timu ya Polisi imesema kamwe haiwezi kukubali kushuka daraja msimu huu.

Polisi imeendelea kusuasua kupata matokeo chanya katika michezo ya Ligi Kuu Zanzibar inayoendelea wakati huu ligi hiyo ikiwa katika mzunguko wa lala salama.

Tangu kuanza kwa msimu huu, Polisi imekuwa haifanyi vizuri baada ya kupokea vipigo saba, sare nne huku ikishinda michezo minne tu na kujiweka katika nafasi ya 11 ya msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar yenye timu 12 ambapo msimu huu zitashuka timu mbili.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu hiyo, Yusuph Sape, alikiri mzunguko wa kwanza kutofanya vizuri na kuahidi mabadiliko katika mzunguko huu wa lala salama. Alisema katika kipindi cha dirisha dogo timu yake ilifanya usajili wa wachezaji sita ambao wataweza kuendana na kasi ya ligi hiyo.

"Timu imebadilika inacheza vizuri baada ya kufanya maboresho katika kikosi chetu, mechi ya mwanzo tu ya mzunguko huu wa pili ndio tulifanya makosa kwa kuwa wachezaji walikuwa bado hawajazoeana, lakini michezo iliyofuata tumefanya vizuri," alisema.

Aidha, alisema licha ya kuambulia sare katika michezo mitatu ya mzunguko huu wa pili, lakini bado matumaini yake ni kutokubali kuiona timu hiyo ikishuka daraja.

Katika mchezo mwingine wa ligi hiyo uliopigwa Uwanja wa Amaan, timu ya Mlandege nayo ililazimishwa sare tasa na Chuoni.

Na kwenye Dimba la Gombani Kisiwani Pemba, vinara wa ligi hiyo, KMKM waliendelea kupunguzwa kasi ya kuukaribia ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kupokea kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa wenyeji, Hard Rock.

# Baraza azua vita Biashara United, Kagera Sugar

**Na Saada Akida**

TIMU ya Kagera Sugar iko katika mipango ya kumng`oa Kocha Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, kuchukuwa mikoba ya Mecky Maxime, lakini klabu yake hiyo imesema kamwe haitakuwa tayari kumwachia mwalimu huyo raia wa Kenya.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti, Katibu Mkuu wa Kagera Sugar, Ally Said, alisema baada ya kumwondoa Maxime walikaa na kujadiliana na hatimaye wakaona Baraza anastahili nafasi hiyo kisha kuanza mazungumzo naye.

Alisema hawajakutana na kocha huyo, lakini wanaendelea kufanya mazungumzo kwa njia ya simu na kama wataafikiana, atakuwa mkuu wa benchi lao la ufundi kabla ya Machi 12, mwaka huu. Alisema Baraza amekuwa chaguo lao namba moja kwa sababu wameridhishwa na kazi ambayo anaifanya tangu msimu uliopita kwa timu anayoifundisha kufanya vizuri na kupata matokeo chanya katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Naye Mwenyekiti wa Biashara United, Seleman Mataso, alisema wanathamini mchango na kazi ya Baraza na watapambana kuhakikisha kocha huyo anaendelea kubaki kukinoa kikosi cha timu hiyo. Alisema kulingana na matokeo wanayoyapata katika timu yao, hawatakubali kumpoteza kocha huyo, hivyo watahakikisha wanapambana na wapinzani wao hao kwa gharama yoyote kuhakikisha kocha huyo anabaki ndani ya kikosi chao.

"Hatuwezi kuona Baraza anaondoka kirahisi rahisi hapa kwetu, hata kama ni suala la dau, nina imani tutapambania hilo, kwa matokeo ambayo tunapata kwa timu yetu, kumuacha kocha anaondoka, mashabiki watatuchukuliaje sisi viongozi katika jambo hilo?" Mataso alihoji.

Gazeti hili lilimtafuta Baraza, ambapo alikiri kufanya mazungumzo na uongozi wa Kagera Sugar, lakini bado hawajafikia makubalinao vizuri kuhusu masuala ya mkataba.

"Tuko katika mazungumzo bado hatujafikia makubaliano yoyote, kuhusu suala la mkataba, kwa sasa tunaendelea kujadili kwa simu hatujakaa pamoja kuzungumza na viongozi hao, ila bado niko na timu yangu ya Biashara United tunaendelea kufanya kazi," alisema Baraza.

# Michezo

Jumatano Machi 10, 2021

Nipashe




Tuchel aanika sababu Pulisic kusugua benchi UKURASA 22

HAWATOKI LEO...



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini. Leo timu hiyo itaikaribisha Tanzania Prisons kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: MAKTABA YETU**

# Mwambusi rasmi sasa arudisha furaha Yanga

●●● Apewa mikoba ya Kaze kwa muda huku mchakato wa kocha mkuu ukiendelea, Aussems atajwa lakini...

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE uongozi wa Klabu ya Yanga umeamua kumrejesha aliyekuwa Kocha Msaidizi, Juma Mwambusi, kuchukua mikoba ya bosi wake, Mrundi Cedric Kaze, aliyetimuliwa baada ya matokeo ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania mwishoni mwa wiki kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

**Klabu ya Yanga ilitangaza kuachana na Kaze pamoja na kuvunja benchi zima la ufundi kwa kile ilichoeleza kuwa ni mwenendo mbaya wa matokeo ya timu hiyo ambayo bado ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na alama 50 baada ya kushuka dimbani mara 23.**

Akizungumza Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Dk. Mshindo Msolla, alisema Mwambusi ataendelea kuinoa timu hiyo wakati huu mchakato wa kutafuta kocha mkuu ukiendelea na wanaimani atafanya vizuri kwa kuwa si mgeni katika kikosi hicho.

"Tunategemea kwamba Mwambusi ataichukua timu wakati tunatafuta mwalimu mkuu, bahati nzuri aliondoka vizuri, aliaga vizuri na klabu imemsaidia katika matibabu amepata nafuu na hana ugeni kwani toka ligi inaanza anayo timu hii mpaka Kombe la Mapinduzi, ni hizi wiki tatu tu yupo nje ya timu, kwa hiyo kurudi kwake kesho ama keshokutwa si jambo geni," alisema Dk. Msolla.

Kuhusu kocha mpya wakati huu tetesi za makocha kibao wakihusishwa kurejea kuinoa akiwamo aliyewahi kuinoa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems na Mhonzi Hans van der Pluijm ambaye aliwahi kuinoa miamba hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam, Msolla alisema mchakato utaendelea kwa kupokea CV (wasifu) wao kabla ya Kamati ya Utendaji kukaa na kupata kocha sahihi.

"Suala la mwalimu sasa tunaendelea na taratibu za kawaida, CV zitaletwa na mtu yeyote yule na tunaimani kwamba zote zitakwenda Kamati ya Ufundi ambapo kuna wachezaji na walimu, watazipitia na kuweka kila kitu mezani na kisha kuwekwa wazi kocha ambaye anatufaa kwa klabu yetu kwa sasa," alisema.

Mwambusi alijiweka kando ndani ya Yanga kutokana na kile ambacho alieleza kuwa hakuwa kwenye afya nzuri na kwamba daktari alimshauri kujitenga na kazi ambazo zitahusisha kelele ama kuzungumza kwa muda mrefu.

Alichukua hatua hiyo baada ya kutwaa Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar wakati huo akiwa msaidizi wa Kaze, ambaye alianza kupata matokeo mabaya huku timu ikishindwa kucheza soka la kuvutia tangu kuondoka kwake.

Hata hivyo, hivi karibuni Mwambusi alisema yupo fiti kiafya na anaweza kureja kazini, jambo ambalo sasa Yanga wameonekana kulifanyia kazi mapema ili kuokoa jahazi.

Kaze anakuwa kocha wa pili kutimuliwa na Yanga tangu kuanza kwa msimu huu wa 2020/21, ikiwa ni baada ya mtangulizi wake, Mserbia Zlatko Krmpotic ambaye naye alifutwa kazi baada ya kuongoza kwenye mechi tano ndani ya ligi.

Zlatko alishinda mechi nne na sare, na wakati anaondoka timu hiyo ilikuwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kama ilivyo sasa kwa Kaze, ambaye ameiacha ikiongoza ligi kwa pointi 50, tano zaidi ya watani zao, Simba waliopo nafasi ya pili lakini wakiwa mechi nne nyuma.

## Simba, Prisons ni visasi na pointi leo

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wanashuka dimbani leo dhidi ya Tanzania Prisons, huku Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes, akisema wachezaji wake wako fiti na tayari kwa ajili ya kupigania pointi ambazo zitaendelea kuwaweka katika mbio za ubingwa.

Simba itakuwa mwenyeji wa mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa leo saa 1:00 usiku, ambapo itataka kulipa kisasi cha kupigwa bao 1-0 katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyopigwa Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga wakati huo ikiwa chini ya Mbelgiji Sven Vandenbroeck.

Kwenye msimamo, Simba iko nafasi ya pili na pointi 45 baada ya kucheza jumla ya mechi 19, huku Tanzania Prisons ikiwa nafasi ya 10 na pointi 27 na tayari wamecheza mechi 21. Akizungumza na Nipashe jana, Gomes alisema baada ya kumaliza mchezo wao dhidi ya Al-Merrikh nchini Sudan, alitoa mapumziko ya siku moja kwa wachezaji ambao walirejea siku inayofuata na kuanza maandalizi ya mchezo huo wa leo ambao anatarajia utakuwa mgumu kwa kila upande.

"Hakuna timu rahisi katika ligi, tumerejea na sasa tumejipanga kwa ajili ya mechi yetu ya ligi dhidi ya Tanzania Prisons, ninaimani utakuwa mchezo wa ushindani kwa sababu kila mmoja wetu anahitaji kupata matokeo mazuri," alisema Gomes.

Kocha Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shaban Kazumba alisema: "Wamejipanga vizuri kwa mchezo huo na hawana majeruhi na wanahitaji kuendeleza kile ambacho walikifanya katika mzunguko wa kwanza."


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042



9 770856 541002 >